epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Machi 6, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581607
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**LEAO HATAKI KUONDOKA AC MILAN** UKURASA 22

**Askari** wadaiwa kumjeruhi mtoto kutumia risasi UKURASA 4




**Zuchu** alikoroga, aadhibiwa, aomba radhi asamehewe UKURASA 3



**Hatari** vijiti vya meno, kuzibua bia kwa meno... UKURASA 4

# Mwinyi: Baba hakuacha wosia pa kumzika

UKURASA 3







Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo aliyemaliza muda wake, Zitto Kabwe (wa pili kulia), akiwaongoza wanachama kuimba wimbo wakati wa Mkutano Mkuu wa chama hicho, Mlimani City, Dar es Salaam jana. Wengine ni Kiongozi wa chama cha NARC kutoka Kenya, Martha Karua (kulia), Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu (wa pili kushoto) na Makamu Mwenyekiti wa ACT Zanzibar, Othman Masoud Othman. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## MKUTANO WA ACT
# Rais kanituma niwaambie uchaguzi huru waja - Kinana

UKURASA 2



# Rais Samia kusikiliza kero kila mwezi kwa kutumia kofia ya CCM

UKURASA 2

**MICHEZO** TFF YATOA SIRI SIMBA, YANGA KUWIKA CAF UK.24 **KABWELA** UK.7

MKUTANO MKUU ACT

# Kinana: Nimetumwa na Rais Samia niwaambie uchaguzi utakuwa huru

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana amewahakikishia watanzania kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani utakuwa wa huru na wa haki.

Amesema dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unakuwa huru na wa haki ili watu wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Alieleza hayo jana alipomwakilisha Rais katika Mkutano Mkuu wa Nne wa Chama cha ACT Wazalendo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

"Kuna sheria na dhamira, unaweza kuwa na sheria nzuri, lakini kama huna dhamira nzuri unaweza kuikanyaga hiyo sheria kama unavyotaka. Unaweza kuwa na sheria mbaya, lakini dhamira nzuri ikitawala, mambo yakawa mazuri.

"Niwahakikishie Rais amekubali uchaguzi ujao uwe wa uhuru na haki. Ninazungumza nikiwa na uhakika. Wapo wenye shaka na kauli hii, lakini wanazo sababu zinazotokana na uchaguzi wa mwaka 2019 na 2020," alisema Kinana huku akishangiliwa na washiriki wa mkutano huo waliopiga kofi.

Aliendelea: "Lazima tuseme ukweli, hofu ya viongozi wenzangu wa vyama vya siasa, asasi za kiraia na viongozi wa dini msingi wake unatokana na yale yaliyojitokeza katika uchaguzi uliopita.

"Ninaomba nikiri Rais Samia ameamua uchaguzi ujao utaachwa wapigakura waamue aina ya kiongozi wanayemtaka."

Kinana ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, alisema Bunge lilifanya marekebisho ya sheria tatu ikiwamo ya uchaguzi hivi karibuni kutokana na dhamira ya Rais Samia. Ndio sababu miswada ya sheria hizo ilipewa muda mrefu wa mjadala bungeni.

Kinana alipongeza Chama cha ACT Wazalendo kutokana na kukubalika kwake nchini. Alikitaja ni chama kichanga ambacho kimesambaa maeneo mbalimbali nchini ndani ya muda mfupi.

"Tumekuwa tunawafuatilia, sisi kama CCM hatuwachukulii kirahisi," Kinana alisema na kuibua tena shangilio ukumbuni.

Alisema CCM inatambua ushiriki wa chama hicho kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa visiwani Zanzibar na iko tayari kukaa nao kiti kimoja kusikiliza na kutafuta haki, uhuru na maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

"Ninawapongeza kwa mnavyoendelea kuimarisha chama, mmepitia kwenye mambo mawili; kwanza ni 'Shusha Tanga Pandisha Tanga', mmefanya bila mafarakano na kazi ikaendelea, halikuwa jambo rahisi," alisema Kinana.

Makamu Mwenyekiti wa CCM huyo alimpongeza Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo aliyemaliza muda wake, Zitto Kabwe kwa kuonesha alichokiita uongozi mzuri, madhubuti na wenye busara na kukiwezesha chama hicho kuwa katika hali ya utulivu.

"Si hilo tu, (Zitto) umekubali kuzingatia matakwa ya katiba mihula miwili, umemaua kukaa pembeni, si kustaafu. Zitto hastaafu, anakaa pembeni, atakuwa mshauri mzuri wa chama chenu.

"Lazima nikiri nimefanya kazi kwa ukaribu na Zitto kupitia Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kwa ajili ya kujenga demokrasia, ninakushukuru sana. Nitachota ushauri wako wa mara kwa mara," alisema Kinana.

Pia alimpongeza mwenyekiti wa chama hicho anayemaliza muda wake, Juma Duni Haji, akisema kuwa uamuzi wake wa kujiondoa kwenye mchakato wa kuwania tena nafasi hiyo unaonesha anajali maslahi ya taifa kuliko mweyewe.

**ZITTO KABWE**

Zitto alitumia mkutano huo kumkaribisha kiongozi mwingine atakayepatikana leo baada ya uchaguzi, akimshauri kuendeleza mema aliyofanya katika uongozi wake.

Alisema chama chao kinafuata misingi ya demokrasia na hivyo wamejitahidi kulinda demokrasia hiyo kwa vitendo, akisisitiza kuagwa kwake ni ushuhuda wa hilo.

"Baada ya kuongoza kwa mulongo mmoja, katiba inanitaka kuondoka na mimi ninataka kuondoka, uongozi ni kama kijiti, lazima tupokezane," alisema Zitto huku akishangiliwa.

Alisema kukua kwa chama hicho kumetokana na viongozi wake kutanguliza maslahi ya chama mbele na kuweka maslahi binafsi nyuma. Ndiyo msingi walioурithi kwa aliyekuwa Mwenyekiti wao, Maalim Seif.

"Ninaondoka katika nafasi hii, imekuwa fahari na heshima kubwa kama kiongozi wenu, kuna wakati nimekuwa na furaha na wakati mwingine nimekuwa na huzuni.

"Wakati wote nimekuwa ninafarijiwa na mapenzi makubwa ya wanachama, ninajiona mwenye baraka kuwa kiongozi wa chama hiki ninachokipenda sana. Siku zote nitakuwa mwenye shukrani sana," alisema Zitto.

Mbali na Kinana, viongozi wengine wa kisiasa walialikwa katika mkutano huo pamoja na maofisa kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, viongozi wa dini na viongozi wa vyama vya upinzani kutoka nchi jirani.

# Samia kusikiliza kero kila mwezi kwa kofia ya CCM

**Na Beatrice Shayo**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, ametangaza kutenga siku moja kila mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero za mwananchi mmoja mmoja kwa kukutana nao katika ofisi za chama hicho, Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda alisema jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa Rais Samia anayafanya hayo kwa lengo la kuwaonyesha viongozi wanavyopaswa kuwajibika katika nafasi zao kutatua kero za wananchi.

"Kwa kuwa ametuelekeza sisi kama chama katika nafasi yetu ya kwenda mikoani na kuwasikiliza wananchi na yale tunayoweza tumewapatia majibu. Kwa mapenzi yake ameridhia kutenga siku moja kwa mwezi kuja katika ofisi zetu za Lumumba (Dar es Salaam) ama Dodoma au ikimkuta yupo Zanzibar atawasikiliza wananchi bila kujali kipato, elimu, fedha, kabila, ukoo wala mtandao gani," alisema.

Alisema Rais ameamua kufanya hayo akiwa na maana kubwa nyingi ikiwamo kudumisha na kuidhinisha kwa vitendo kwa kuwataka viongozi aliowateua kuwasikiliza na kutatua kero za wananchi.

"Mwananchi atakayepata nafasi ya kumwona Rais Samia katika ofisi zetu za chama kama hiyo siku itaangukia Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar, atamweleza kama alikwenda katika ofisi za serikali na hakupatiwa majibu ili ajue watendaji wake wanafanya kazi au wanakula mshahara bure," alisema.

Alisema sababu ya pili ni ya kumuenzi Hayati Rais Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa na utamaduni huo wa kuwasikiliza wananchi na kwa kuwa yeye ni mwanafunzi wake ameamua kuyafanya kwa vitendo yale mema mengi ambayo alikuwa akiyafanya.

Makonda alisema jambo lingine ni mujibu wa ilani ya CCM na katiba yao imewapa nafasi ya kutumia vyeo vyao kwa manufaa ya wengine.

Aidha, alisema tathmini waliyoifanya ya ziara katika mikoa 23 wamefanya mikutano 247 kupokea kero 2,000 na kwamba wamebaini dhuluma katika sekta ya ardhi inayofanywa watu wenye fedha kwa kushirikiana na watumishi wa umma kusababisha wananchi kuichukia serikali.

"Jambo la kwanza tulilolibaini ni mioyo ya Watanzania wengi imeumizwa na dhuluma na hii imegawanyika katika maeneo mengi au kwenye sekta nyingi na chama tawala tuna wajibu wa kuweka mkazo wa kupambana na dhuluma hiyo," alisisitiza.

Alisema kilio cha watu kunyang'anywa maeneo yao walio na haki na wenye nguvu ya fedha imetawala.

"Kilio cha watu kupewa nyaraka au hati feki kimetawala katika eneo hilo tulitoa maelekezo na yalifanyiwa kazi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, tumeziona jitihada zake na utiifu wake kwa chama," alisema Makonda.

Makonda alisema wale wote waliodhulumu na kunyang'anya haki za wananchi wasisite kuchukua hatua hata kama zina maumivu ziwe fundisho ili kumlinda mnyonge na maskini wa taifa hili asikandamizwe na wenye fedha na wenye mitandao mikubwa ya kujuana na watu wanaowalinda.

Aidha, Makonda alisema katika ziara hiyo wamebaini tatizo lililopo la viongozi kutokutatua kero za wananchi ndio maana kila wanapokwenda wananchi wanaeleza changamoto zao hazijafanyiwa kazi.

Alisema viongozi wanatakiwa kutambua ofisi walizokuwa nazo sio zao ni za umma kutokufanyia kazi matatizo ya wananchi ni kuongeza shida na kusababisha wanaichukulia serikali.

Alisema kutokutatuliwa kwa changamoto za wananchi ofisi za CCM Lumumba Dar es Salaam na Dodoma inapokea idadi ya malalamiko kwa siku kuanzia 100 hadi 200.

"Maelekezo ya chama kila aliye na nafasi ana wajibu wa kutatua changamoto aliyopelekewa na wananchi na afahamu kuwa ile ofisi siyo yake ni ya umma," alisema.

Aidha, Makonda alisema wamebaini masuala ya ukatili wa watoto, mama na unyanyasaji katika maeneo mbalimbali na hilo wameliwekea utaratibu ili kutatua changamoto hiyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
05.03.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **07.03.2024 hadi 14.03.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga** kuelekea **Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB54202 DS00TG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro,** Barabara ya Mandela gari litasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***




Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation For Civil Society (FCS) anayemaliza muda wake wa uongozi, Francis Kiwanga (kulia), akikabidhi nyaraka za ofisi kwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Taasisi hiyo, Justice Rutenge katika hafla ya makabidhiano ya uongozi wa taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya FCS, Ally Laay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mzee Mwinyi hakuacha wosia azikwe wapi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa mzazi wake, Rais mstaafu wa awamu wa pili, Mzee Hassan Mwinyi, wakati wa uhai wake hakutoa wosia wowote kuhusu mahali pa kuzikwa baada ya kifo chake.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika hitma maalum (dua) iliyoandaliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyofanyika Masjid Zinjibar, Mazizini nje ya mji wa Zanzibar. Msikiti huo ndimo ulipo-saliwa mwili wa marehemu Mzee Mwinyi kabla ya kwenda kuzikwa kijijini kwao, Mangapwani mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema mzee wake alipozidiwa na wakati akipatiwa matibabu Uingereza pamoja na wakati wote akiugua, alikuwa akisisitiza mara kwa mara kuwa arejeshwe Zanzibar, akiwa na maana kuwa kifo chake kimfike akiwa Zanzibar na kuzikwa visiwani hapa.

Hata baada ya kurudi Dar es Salaam, alisema aliendelea kusisitiza hilo kwamba arejeshwe Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya haikuwezekana kwa sababu ya uangalizi wa madaktari Hospitali ya Mzena.

"Kuna mengi yalisemwa katika mitandao kuhusu usia. Ndugu zangu, usia (wosia) mtu hutoa kwa familia yake na si kwa watu wengine. Sie ndio tunaojua alichokiusia lakini tunasema yote yanayosemwa tutavumilia," alisema Dk. Mwinyi.

Pia alisema kuna mengine mengi yatasemwa lakini aliitaka familia yake kuwa na subira licha ya mengine yatakayosemwa yatakayomlenga yeye kama Rais wa Zanzibar.

Alisema fundisho kubwa alilolipata kwa mzazi wake huyo ni unyenyekevu na subira licha ya kusemwa vibaya wakati wa uhai wake na baadhi ya watu na watu hao ni wale aliowapa uhuru lakini hakuwa akijibu tuhuma hizo ambazo si za kweli bali ni za kutungwa.

"Moja ya mafundisho tuliyoyapata kwa mzazi wangu ni Subira. Namshukuru mzee wangu kwa kutupa mafunzo mema,"alisema.

Alisema hulka ya Mzee Mwinyi ilikuwa kumheshimu kila mtu, wakubwa kwa wadogo na alikuwa na marafiki mpaka watoto wadogo na pia alikuwa na uhusiano mzuri na kila mtu.

Dk. Mwinyi alisema binafsi alikuwa akienda kwa baba yake, alikuwa lazima asimame ndipo amsalimie kwa kumpa heshima yake kutokana na wadhifa wake wa urais wa Zanzibar licha ya kuwa ni mtoto wake.

# Zuchu alikoroga, aadhibiwa, aomba radhi asamehewe

**Na Elizabeth Zaya**

MANENO yanayodaiwa kutokuwa na staha kulingana na mila na desturi za Kizanzibari, yameelezwa kumponza msanii wa muziki wa kizazi kipya, Zuhura Othman (Zuchu), kufungiwa kufanya shughuli za muziki visiwani humo kwa miezi sita na kutozwa faini ya Sh. milioni moja.

Akitumbuiza katika tamasha lake alilofanya Februari 24, mwaka huu, Kendwa Mkoa wa Kaskazini Unguja, lililobeba jina la Usiku wa Fullmoon, Zuchu anadaiwa kutumia maneno yasiyo na staha yakiwamo matamshi na kuonyesha ishara mbaya kinyume cha maadili.

Akitoa taarifa ya kumfungia msanii huyo jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa, Sensa, filamu na Utamaduni Zanzibar, Omar Abdalla Adam, alisema imekuwa tabia ya msanii huyo kuimba nyimbo zisizo na maadili, kutofuata misingi na hazina njema kwa jamii ya Wazanzibari.

Pia alisema licha ya msanii huyo kutokuwa na usajili Zanzibar, amekuwa akiendesha shughuli zake za sanaa visiwani humo bila kupata kibali.

"Baraza lina wajibu wa kusimamia mila, silka, desturi na utamaduni wa Mzanzibari. Kwa hiyo limatamka rasmi kumfungia Zuhura kufanya shughuli yoyote ya sanaa kwa Zanzibar kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Machi 5, mwaka huu," alisema Adam.

Mbali na adhabu hiyo, pia msanii huyo ametakiwa kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa baraza hilo pamoja na kuandika barua ya kuomba radhi na kuthibitisha kwamba hatafanya kosa hilo ndani ya kipindi alichofungiwa.

Katika barua yake ya kuomba radhi, Zuchu alisema hakuwa na nia mbaya ya kuleta mmonyoko wa maadili wala taharuki kwa yeyote bali alikuwa kwa lengo la kutoa burudani njema na kufurahisha mashabiki wake wote.

"Ninatoa ahadi leo kufanya kazi na timu yangu ili kuhakikisha matukio kama hayo hayatokei tena kwenye matamasha yajayo. Nawaomba radhi tena kwa jamii na Baraza la Sanaa ambao ndio walezi wangu," alisema Zuchu.

Zuchu alitoa kauli hiyo jana saa chache baada ya baraza hilo kutangaza kumfungia kufanya shughuli zote za sanaa visiwani Zanzibar sambamba na kupiga marufuku nyimbo zake kupigwa katika redio na televisheni za visiwani humo kwa muda aliofungiwa.

Baada ya msanii huyo kuomba radhi na barua yake kuwekwa mtandaoni, baadhi ya watu walitoa maoni tofauti.

"Zuchu nampenda lakini akiwa kwenye 'show' hajiheshimu na kazi yake. Yeye ni michambo tu," alisema mmoja wa wachangiaji aliyejitambulisha kwa jina la Sweetlylizzy.

Yef2007 aliandika: "Lazima uwe na uchaguzi wa maneno ya kutumia. Binafsi nilisikitika sana kwenye hicho anachosema kibwagizo(anakitaja) hongera kwa kutambua kosa na kuomba radhi."

Naye Sylus Shany aliandika: "Hiyo radhi ni ya kinafiki kwani hukujua kama(anataja neno), ilikuwa lugha chafu, ulifanya kusudi. Tulishazoea wewe na huyo(anamtaja).

"Utukane kesho uje uombe radhi...mnafanya wazazi watukanwe kila siku, mama yako kaimba mziki miaka sijui 40 hatujawahi hata kusikia akitamka(anataja neno), acheni kujitoa ufahamu," aliandika hivyo Digala.



# Daktari aonya matumizi vijiti kufungua bia, soda kwa mdomo

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Msaidizi wa Huduma za Kinywa na Meno katika Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, amezitaja tabia kadhaa zinazosababisha afya ya kinywa na meno kuwa duni.

Baadhi ya tabia hizo ni matumizi ya vijiti vya kuchokonolea meno ('toothpick') baada ya mlo, kufungua vifuniko vya soda au bia kwa kutumia meno na kufanya ngono kwa njia ya mdomo.

Amesema pia tabia nyingine kama vile kunyonya vidole, imekuwa ikiendelea katika baadhi ya watu kwenye jamii na kuonya kuwa inasababisha mdomo wa meno kutofunga siku za baadaye.

Dk. Nzobo aliyasema hayo jana akizungumza na Nipashe, kuhusu afya ya kinywa na meno kwa lengo la kutoa elimu kwa umma.

"Katika jamii ya Kitanzania, kumekuwapo na tabia mbalimbali ambazo zimegeuka kuwa mazoea ingawa hazifai kuigwa. Tabia hizi zimekuwa zikileta madhara makubwa kwenye kinywa na meno," alisema.

Dk. Nzobo alisema tabia iliyojengwa na baadhi ya watu kufungua vifuniko vya soda au bia kwa kutumia meno, haifai kuendelezwa.

"Watu wengi wamekuwa wakifungua vifuniko vya soda au bia kwa kutumia meno na wengi wao wamekuwa wakiyapasua au kuyavunja meno yao kwa kufanya jambo hili.

"Jino likipasuka huwa linapasuka mpaka kwenye mzizi wake na hivyo kusabisha ling'olewe. Tunashauri watu watumie vifungulia chupa (opener) wanapotaka kunywa soda au bia," alisema.

Aliitaja tabia ya nyingine ya pili isiyofaa ni kunyonya vidole, akisema baadhi ya watu wazima na watoto wamekuwa na tabia ya kunyonya videlo hasa dole gumba la mkononi.

"Tabia hii huanza toka toka utotoni na baadhi ya watoto wanashindwa kuiacha na kuendelea kunyonya dole gumba hadi wakiwa watu wazima. Tabia hii ya kunyonya dole gumba husababisha meno ya mbele ya taya la juu na chini kushindwa kukutana mtu anapofunga mdomo.

"Ukimwambia ng'ata meno, basi meno ya nyuma yatakutana, lakini meno ya mbele kamwe hayawezi kutana. Hii husababisha kuharibu muonekano mzuri wa sura ya mtu huyo.

"Mzazi ambaye ana mtoto ananyonya dole gumba na ameshindwa kuacha tunamshauri ampeleke kwa Daktari wa Kinywa na Meno atamsaidia mtoto huyo kumpatia tiba ya kuacha kunyonya dole gumba," alisema.

Daktari huyo anataja tabia ya nane isiyofaa ni kama vile matumizi ya 'toothpick' akisema watu wengi mara baada ya kumaliza kula hasa nyama, huchukua toothpick na kuanza kuchokonoa kwenye meno.

"Kutoa nyama zilizonasa kwa kutumia 'toothpick' kunaharibu fizi na meno. Toothpick zilizo nyingi ni nene na hazifai kwa afya ya jino na fizi. Matumizi ya 'toothpick' mara kwa mara husababisha kutengeneza uwazi mkubwa kati ya jino na jino, hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo la vyakula kunasa sehemu hiyo.

"Vyakula vinapozidi kunasa kwa wingi hukaribisha magonjwa ya fizi na hata kuozesha jino karibu kwenye kiungio chake. Tunashauri watu watumie uzi maalumu uitwao Dental floss kutoa vyakula vinavyonasa kwenye meno yao," alisema.

Pia alisema tabia ya nne isiyofaa kuwa ni, baadhi ya wapenzi kunyonya sehemu za siri za mwanaume au mwanamke. "Tabia hii imeshika sana kasi kwenye jamii, hasa wakati wa kushiriki tendo la ndoa.

"Unaponyonya sehemu za siri za mwezi wako unajiweka kwenye hatari ya kuambukizwa virusi vinavyosababisha saratani ya koo na wengine kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa mdomoni.

"Kama kuna ulazima sana wakufanya mapenzi mdomoni basi watu watumie kondomu za mdomoni," alisema Dk. Nzobo.

## NMB yaunganisha ATM zake na ATM za benki za Umoja Switch

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB na Kampuni ya UBX Tanzania Limited, inayoendesha mtandao wa ATM wa Umoja Switch zimeingia katika ushirikiano wa kimkakati unaounganisha benki washirika kwenye mtandao mmoja wa ATM.

Ushirikiano huo wa kimkakati ni hatua muhimu kwa sekta ya kibenki Tanzania kwa kuwa unaunda mfumo mpana wa matumizi ya pamoja ya mashine za kutolea fedha (ATM).

Ubia huu wa kimkakati unapelekea kuunganishwa kwa mafanikio makubwa ATM 280 za Umoja Switch na ATM za NMB zaidi ya 700, ikiashiria zama mpya ya upatikanaji ATM na ufanisi katika huduma za kibenki nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema: "Tumefurahishwa na ushirikiano huu kwani unawawezesha wateja wetu kupata huduma za kibenki kwa urahisi.

"Sasa wateja wetu kwa kujinafasi wanaweza kupata huduma za kibenki kwa unafuu na uhakika kwenye ATM zaidi ya 1,000 kote nchini. Hiyo ndiyo faida ya ushirikiano huu.

"Ushirikiano huu pia unakwenda kupunguza gharama za uendeshaji kwa benki shiriki kwani miamala yote inayofanyika nchini haitakuwa na ulazima tena wa kuchakatwa nje ya nchi," aliongeza.

Alisema kuwa kupitia ushirikiano huo, watanzania watapata manufaa ya upatikanaji huduma za ATM. Wateja wa benki zote 17 za Umoja Switch na wale wa Benki ya NMB watafanya miamala na kupata huduma za kibenki wakati wowote kupitia mtandao wa ATM zaidi ya 1,000.

Alisema gharama pia zitapungua kwa kuwa ushirikiano huo unaongeza ufanisi na kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za miamala kwa wateja wa benki zote 17 watakaotumia ATM za NMB na wateja wa NMB watakaotumia ATM za Umoja Switch kwa zaidi ya asilimia 70.

Manufaa mengine kwa mujibu wa Zaipuna ni ujumuishi wa kifedha - ubia huo ukitarajiwa kuongeza matumizi ya kadi kwenye ATM nchini na kupunguza foleni katika matawi na hivyo kuwa njia mbadala ya kuimarisha ujumuishi rasmi kifedha nchini.

"Pia kutakuwa na ufanisi wa benki kwa sababu benki zinazoshiriki zitafikia maeneo ya pembezoni ambayo awali yalikuwa magumu kwa taasisi moja kuyafikia kwa kuweka ATM.

"Gharama za uendeshaji pia zitapungua kwa sababu ushirikiano huo utazipunguzia benki shiriki gharama za uendeshaji. Miamlala yote itakayofanyika nchini haitahitajika tena kuchakatwa nje ya nchi, badala yake, hilo litafanywa na mtandao wa NMB na UBX, hivyo kupunguza gharama kubwa za uendeshaji za hapo awali," alisema.




Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande (katikati), akizungumza baada ya kuzindua ushirikiano kati ya Benki ya NMB na Kampuni ya UBX inayosimamia ATM za Umoja Switch zinazohudumia benki zingine 17, jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wanaotumia kadi za Umoja Switch wataweza kutumia mashine za kutolea pesa za NMB bila gharama za ziada na wa NMB hivyo hivyo na wa Umoja. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa UBX, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Ubia huo ulizinduliwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande ambaye alisema ushirikiano wa NMB na UBX unaongeza thamani kubwa katika juhudi za serikali za kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma rasmi za kifedha kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Chande alishauri benki zingine kujiunga na mtandao wa ATM wa NMB na Umoja Switch.

Mwenyekiti wa Bodi ya UBX, Sabasaba Moshingi, alisema Umoja Switch ilipoanzishwa mwaka 2006 ilikuwa na wanachama sita na ATM 30 tu ambazo hazikuweza hata kuwahudumia wateja zaidi ya 2,000.

Alisema washirika wa ushirikiano huo wa kimapinduzi sasa wanaweza na kwa gharama nafuu kuzifikisha kazi za msingi za tawi katika mazingira ya pembezoni kabisa na yenye changamoto.

"Kwa kweli ushirikiano huu unaashiria dhamira ya pamoja ya kupunguza pengo la kidijitali na kifedha. Kupitia teknolojia na ushirikiano, tunalenga kuwawezesha watu ambao hawahudumiwi vya kutosha na hivyo kuhamasisha ukuaji wa uchumi," alisema.

## Askari wadaiwa kumjeruhi mtoto wakitumia risasi

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

NEEMA Nassoro (16) mkazi wa Kijiji cha Murwambe, Tarime mkoani Mara, amejeruhiwa kwa kupigwa risasi na watu wanaodaiwa kuwa ni askari wa mgodi wa Barrick North Mara wakati akiwa katika kibanda cha biashara ya chakula cha mama yake mzazi.

Tukio linadaiwa kutokea mwishoni mwa wiki iliyopita katika eneo la Murwambe, Nyamongo wilayani humo. Inaelezwa kuwa askari hao walifika katika eneo hilo na kuanza kurusha risasi ovyo ndipo ikampata binti huyo.

Mama mzazi wa Neema, alisema waliona gari la askari likiwa limesimama maeneo ya kibanda chake na ghafla wakasikia milio ya risasi ikilenga katika kibanda hicho ndipo alipokimbilia ndani.

"Baada ya kuingia ndani nilikuta zile risasi walizokuwa wakipiga kumbe iko iliyompata mwanangu niliyemkuta amelala chini na damu zinatoka huku akilia. Nikambeba mgongoni kumkimbiza katika Kituo cha Afya cha Nyamongo ili kupata huduma zaidi," alisema.

Pia alisema wakati huo aliacha biashara yake na aliwaacha watoto wake wengine bila uangalizi na hakujua kilichoendelea nyuma.

Daktari wa kitengo cha mifupa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mara, Elias Nguti, alisema alimpokea baada ya kupata rufani kutoka katika Hospitali ya Nyamwanga ya wilayani Tarime.

Pia alisema alifikishwa katika Hospitali ya Nyamwanga akitokea Kituo cha Afya cha Nyamongo alichopelekwa baada ya kujeruhiwa miguu yake miwili. Alisema baada ya kumfanyia uchunguzi wa kipimo cha mionzi (X-Ray) walibaini kuwa na vipande vya chuma kwenye mguu wa kulia.

Alitaja maeneo mengine kuwa ni sehemu ya viungio vya mguu wa kushoto, sehemu ya unyayo na baada ya kubaini hali hiyo walimfanyia upasuaji na kumtolea vyuma hivyo.

Kutokana na tukio hilo, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, aliitisha mkutano wa hadhara na wananchi wa eneo hilo na baadhi ya mashuhuda walisema tukio hilo si la kwanza kutokea.

Walisema tukio kama hilo lilitokea uwanja wa ndege wa Buturo kwa askari wa mgodi kumjeruhi mtoto wa darasa la tatu kwa kumpiga pia risasi mguuni.

Waitara alisema mama huyo ameharibiwa kibanda, mtaji wake umepotea na mtoto wake anaumwa, hivyo askari waliotenda kosa hilo, wanapaswa kuwajibishwa kwa kulipa gharama zote za uharibifu na kuchukuliwa hatua kama wahalifu wengine.

# Mbinu mpya wezi pikipiki hadharani

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema kuwa wezi wa pikipiki huzibadilisha namba za usajili ili kujimilikisha na kuzikodisha kwa mkataba kwa watu mbalimbali kwa lengola kujipatia kipato kila siku.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa takwimu za operesheni endelevu ya kuzuia uhalifu zilizofanyika kuanzia Januari mwaka jana hadi sasa, ambapo alieleza walikamata watu watatu waliojimilikisha pikipiki 32 za wizi.

"Tunaendelea na operesheni maalum ya kuzuia vitendo vya uhalifu na kukamata watuhumiwa mbalimbali wakiwamo wezi wa pikikipi na kukamata pikipiki zilizoibwa maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam na mikoa ya jirani.

"Operesheni hii ilianza Februari 6, 2024 na inaendelea mpaka sasa. Tumemkamata Omari Mlopa (28), mkazi wa Mlandizi na wenzake wawili wakiwa na pikipiki 32 zilizoibwa na baadaye kuzifanya zao kwa kuzikodisha kwa mikataba kwa watu mbalimbali na kujipatia fedha kila siku," alisema.

Kamanda Muliro alisema uchunguzi wa awali uliofanywa na Jeshi la Polisi Kanda hiyo umebaini kuwa, watuhumiwa hao walibadilisha namba za usajili za pikipiki hizo na kuweka namba bandia ili zisitambulike.

Alisema tayari pikipiki 13 kati ya hizo zimetambuliwa na wamiliki.

Akitoa takwimu za wanaokiuka sheria za usalama barabarani hasa waendesha bodaboda, Kamanda huyo alisema mwezi Januari hadi Desemba 2023, makosa ya pikipiki yaliyokamatwa ni 179,174.

Alisema kati yao, walioandikiwa faini za papo kwa hapo ni 178,937, waliofikishwa mahakamani walikuwa ni 237, waliohukumiwa adhabu ya kulipa faini ni 236 na mmoja alihukumiwa kifungo.

"Katika kipindi cha Januari hadi Februari 2024, makosa ya pikipiki yaliyokamatwa ni 36,775, walioandikiwa faini za papo kwa hapo ni 36,754, waliofikishwa mahakamani ni 14, na mashauri saba yapo kwenye Ofisi ya Mashitaka ya Taifa," alisema.

Kamanda Muliro alisema katika operesheni hiyo baadhi ya makosa ambayo yamekuwa yakijirudia kwa waendesha pikipiki na bajaji ni, kutovaa kofia ngumu, kupita taa nyekundu, ulevi, kuzidisha abiria, kupita barabara za mabasi yaendayo haraka pamoja na kupakia kwenye taa za kuongozea magari.

# Kampeni EATV Mwanamke Kinara 2024 yaanza rasmi

**Na Christina Mwakangale**

VITUO vya EATV na EA Radio kwa kushirikiana na wadau, vimezindua kampeni ya 'EATV Kinara 2024' ambayo inalenga kuwatambua na kuwainua wanawake wanaotoa mchango mkubwa kwenye jamii nchini, ikiwamo kiuchumi.

Mratibu wa kampeni hiyo, Bhoke Egina, alisema haya jana, katika uzinduzi wa kampeni hiyo kwenye ofisi za kituo hicho, Mikocheni, Dar es Salaam.

"Tumekuwa na mradi huu kwa miaka mingi lakini kuizindua hapa ni mwaka wa tatu. Naona familia inakuwa kubwa tukiwa na wanaotuunga mkono, mwaka 2022 tulizindua hapa (EATV).

"Na mwaka 2023 na 2024 tumefanya vivyo hivyo hapa hapa, na mwaka huu tutafanya tukio la mradi huu Machi 2, mwaka huu jijini Dar es Salaam. Mradi huu unasababu za kuuanzisha, kutambua wanawake ni sehemu kubwa katika jamii.

"Wanafanya vitu vikubwa na muda sasa wanatambuliwa nasi EATV na EA Radio tunawatambua. Ukiangalia hapa Mkurugenzi Mtendaji (Regina Mengi) hapa ni mwanamke. wafanyakazi pia wengi ni wanawake na viongozi wengi ni wanawake wanafanya kazi nzuri," alisema.

Alisema kwamba kuna vipindi maalum ambavyo vinawatambua wanawake kupitia vituo hivyo, akikitaja cha DADAZ kinachorushwa na EATV pamoja na cha MAMA MIA kinachokwenda hewani kupitia EA Radio.

"Vipindi vyetu kauli mbiu ni kumuinua mwanamke aweze kujitegemea, tunafahamu ukiinuka na kuwa si tegemezi kiuchumi unaweza kufanya maamuzi, huwezi kupata ukatili," alisema Bhoke.

Alisema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, mwaka huu, vituo hivyo kwa kushirikiana na ORYX Energies, vitatoa nishati ya mafuta ya gari bure, kuanzia asubuhi hadi jioni, kwa ambao watatazama EATV na kusikiliza EA Radio.

"Vigezo na masharti vitazingatiwa, wewe si kinara dereva mwanamke uwe unaendesha bajaji, bodaboda, gari. Tutatoa mafuta bure, tutakupa mafuta bure, tutaihudumia siku yako," alisema Bhoke.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akionyesha kwa waandishi wa habari, jijini humo jana, baadhi ya pikipiki zilizokamatwa katika operesheni endelevu ya kuzuia uhalifu. **PICHA: MPIGAPCHA WETU**

# Anayedaiwa kunajisi afariki akipatiwa matibabu

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi, limesema kuwa mtuhumiwa aliyetambulika kwa jina la Christoper (56) wa tukio la kumnajisi mtoto wa miaka saba, amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu kutokana na kupigwa na wananchi wenye hasira kali kabla ya kufikishwa kituoni.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Kaster Ngonyani, alisema mtu huyo anadaiwa kutenda tukio hilo katika kijiji cha Dilifu, manispaa ya Mpanda.

Kamanda Ngonyani alisema baada ya baba wa mtoto huyo kumkuta akitenda tukio hilo, aliita majirani ambao walimkamata na kumpiga mawe kisha kujeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili wake.

Tukio la mtoto huyo kunajisiwa lilitokea mwishoni mwa mwezi uliopita. Wakati wazazi wa mtoto huyo wakiwa shambani, ndipo mtuhumiwa ambaye ni jirani wa familia hiyo, alifanya ukatili kwa mtoto huyo katika jengo ambalo halijamalizwa kujengwa nyumbani kwao na mtoto huyo.

Akisimulia tukio hilo, baba mzazi wa mtoto alisema alipotoka kazini alisikia kama kuna watu ndani ya nyumba na alipochungulia, alikuta mtoto wake amelazwa chini akiwa hana nguo na mwanamume huyo akiwa amevua suruali yake nusu amemlalia mtoto. Baada ya hapo, aliita majirani wamsaidie ambao walimkamata na kumfikisha serikali ya mtaa.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Msangama, Regina Josephat, alithibitisha kumpokea mtuhumiwa huyo akiwa amejeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili kisha alimkabidhi polisi.

Mwenyekiti huyo alisema tukio hilo ni la pili kutokea katika eneo hilo huku akidai chanzo kikubwa cha matukio hayo hasa kwa watoto ni jiografia ya eneo hilo nyumba kuwa mbalimbali na kuzungukwa na machimbo ya dhahabu pasipokua na ulinzi shirikishi.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi Mkoani Katavi, limewakamata watu 107 kwa tuhuma mbalimbali na kwamba kati yao, sita wanadaiwa kufanya mauaji.

Ngonyani alisema watuhumiwa 24 kati yao wanajihusisha na wizi, unyang'anyi, uporaji, uvunjaji na uzururaji na wengine 35 wakiwa na nyara za serikali ambazo ni nyamapori aina ya nyati, pofu, twiga zenye jumla ya kilo 42 pamoja na ngozi ya simba na magamba ya kakakuona.

Alisema watuhumiwa 29 wengine wamekamatwa wakiwa na pombe haramu lita 178 na mtambo mmoja wa kutengeneza pombe ya moshi huku saba wakiwa na dawa za kulevya aina ya bangi kete 39 na gramu 200.

Pia alisema watuhumiwa wanne kati yao wanajihusisha na wizi wa mifuga ambapo wamekamatwa wakiwa na ng'ombe 10 zenye thamani ya Sh. 6,712,000 zilizoibwa maeneo mbalimbali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wajenge utamaduni kuheshimu maoni ya wataalamu

**MARA** kwa mara wataalamu wa sekta anuwai wamekuwa wakitoa ushauri kuhusu matumizi ya vitu mbalimbali zikiwamo athari ambazo zinaweza kuwapata watumiaji hao wasipozingatia mambo hayo. Miongoni mwa wataalamu hao ni wa sekta ya afya ambao wamekuwa wakiweka kinagaubaga kuhusu athari za matumizi ya mambo mbalimbali kwa afya zao.

Wiki hii kwa mfano, madaktari bingwa wa tiba ya masikio, pua na koo pamoja na kinywa na meno, walibainisha athari za matumizi ya vitu mbalimbali. Mmoja ni daktari bingwa wa masikio, pua na koo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) - Mloganzila, Dk. Jonas Ndasika, ambaye alionya kuwa kuchangia spika za kuweka sikioni (earphone) ni chanzo cha maambukizi katika masikio.

Kwa mujibu wa daktari huyo, kusikiliza sauti kubwa kupitia vifaa hivyo pia kunaweza kusababisha upotevu wa usikivu kwa kuwa kunaathiri mishipa ya masikio. Aliweka bayana kuwa 'earphone' inaathiri moja kwa moja mishipa ya usikivu na kwamba kelele nyingi zinaweza kumweka mtu katika hatari ya kupoteza usikivu.

Daktari huyo alifafanua kuwa matumizi ya vifaa hivyo vya usikivu kwa muda mrefu ni hatari zaidi kwa kuwa husababisha unyevunyevu katika mfereji wa sikio huku akionya kuwa wanaochangia vifaa hivyo, wanayaweka masikio yao katika hatari ya kushambuliwa na bakteria au fangasi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Pia alionya matumizi ya pamba katika usafishaji sikio kwa kutumia pamba zenye vijiti kwa kuwa husababisha nta laini inayolinda sikio kusukumwa ndani. Alishauri kuacdha matumizi ya pamba hizo kwa kuwa sikio lina uwezo wa kujisafisha na kusisitiza kuwa kitaalamu haishauriwi kufanya hivyo.

Mbali na mtaalamu huyo bingwa katika masuala ya afya, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Kinywa na Meno katika Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, ameibua hoja ya matumizi ya vijiti kuondoa mabaki yaliyo kwenye meno baada ya kumaliza mlo pamoja na kutumia meno kufungua vifuniko vya bia na soda.

Tabia hizo ambazo zimekuwa za kawaida miongoni mwa jamii, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, zina athari kubwa kwa afya ya kinywa na meno. Ni dhahiri kwamba katika maeneo mengi, baadhi ya watu wamekuwa wakifungua chupa kwa kutumia meno pindi mhudumu anapochelewa hali ambayo imeelezwa kuwa ni hatari kwa afya ya jamii.

Kwa kufanya hivyo, mtaalamu huyo anasema wengi wamekuwa wakiyapasua au kuyavunja meno yao huku akibainisha kuwa jino likipasuka huwa linapasuka mpaka kwenye mzizi, hivyo kusabisha ling'olewe.

Daktari huyo, kuhusu matumizi ya vijiti baada ya kumaliza kula, nayo imekuwa ya kawaida kwa watu wengi bila kujua athari zitokanazo na kufanya hivyo. Anabainisha kwamba kutoa nyama zilizonasa kwa kutumia 'toothpick' kunaharibu fizi na meno kwa sababu vijiti vingi ni vinene na havifai kwa afya ya jino na fizi hali ambayo mara kwa mara husababisha kutengeneza uwazi mkubwa kati ya jino na jino, hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo la vyakula kunasa sehemu hiyo.


Kutokana na matumizi hayo, vyakula vinapozidi kunasa kwa wingi hukaribisha magonjwa ya fizi na hata kuozesha jino karibu kwenye kiungio chake, hivyo kushauri kutumia uzi maalumu uitwao 'dental floss' kutoa vyakula vinavyonasa kwenye meno.

Kutokana na ushauri huo wa wataalamu wa afya, ni vyema Watanzania wakajenga utamaduni wa kuheshimu na kufuata ushauri wao ili kulinda afya zao. Kama wahenga wasemavyo mdharau mwiba mguu huota tende, iwapo ushauri huo hautafuatwa, kuna uwezekano mkubwa wa jamii kukumbwa na madhara makubwa kiafya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Watanzania tujali, tuthamini vyetu

**TAIFA** hili lina mazuri mengi ya kujivunia ndiyo maana viongozi waliopo na waliotangulia wamelionyesha hilo.

Viongozi hao ni pamoja na Mzee Ali Hassan Mwinyi , aliyekienzi, kukikuza na kukithamini Kiswahili na sasa kinatumika dunia nzima.

Aidha, aliupenda utamaduni wa Zanzibar kwa kuikuza taarabu asilia na kukumbusha kuwa lazima kuenzi vyetu.

Kama alivyokuwa Mzee Mwinyi, hayati John Magufuli, aliyeongoza awamu ya pili, aliacha mengi ya kuhamasisha Watanzania kupenda na kuthamini vyao na utamaduni wao.

Aliwahi kusema kuwa Tanzania ina viwanda na inaweza kuzalisha bidhaa muhimu wafanyabishara wawekeze na kuongeza thamani bidhaa ili kuendelea kuthamini vyetu.

Magufuli aliwahi kukiri na kutoa kauli ya kishujaa akisema si sisi wala Tanzania yetu ni masikini, ni miongoni mwa mataifa wafadhili kwani hapa kuna kila kitu tena kilicho bora.

Aidha, alikumbusha kuwa kampeni za tiba na kinga za maradhi siyo lazima zitumie dawa na mbinu za kutoka nje kwani hata dawa za asili zitokanazo na mizizi, majani na magome kutoka kwenye misitu yetu zinafaa.

Ndizo zilizotumika kujikinga na kujitibu na maradhi ya UVIKO-19 kwenye kupiga nyungu na kujifukiza .

Aliwashauri Watanzania kutumia dawa hizo za majani na miti kujifukiza, kunywa na kuchanganya na vinywaji kama chai kwani kirusi hicho cha korona kisingeweza kukaa karibu na mwili na hata vitu vya moto.

Hata sasa, Rais Samia Suluhu Hassan, anasimama kijemadari kuzidi kuwakumbusha watu kuthamini Utanzania na vitu vyake, kiongozi huyu akisimamia kuendeleza Kiswahili na kutangaza utalii wa taifa.

Kwa kuthamini nchi yake amewaongoza kuionyesha Tanzania kwa upana zaidi na watu wengi wakaitambua kwani alishirikiana na wasanii kuandaa filamu ya The Royal Tour.

Ilikuwa ni ukweli na uhalisia wa kutangaza kwa kasi barani Afrika na duniani kote vivutio utalii na vitu vya maajabu vinavyopatikana Tanzania.

Ameifahamisha dunia kuwa taifa analoongoza lina fahari kubwa na mengi ya kujivunia na kunadi kupitia picha hiyo inayoonyesha ukweli na uhalisia.

Tanzania ina mengi kuanzia milima upo Kilimanjaro, bahari, mito, mabonde, madini,wanyama, misitu asilia, ndege na maliasili nyingi zinazotambulika kwa ubora Afrika.

Kuna visiwa maridhiwa kuanzia Zanzibar, Mafia na Pemba kwenye mengi ya kujivunia.

Kwa maana hiyo, Watanzania waamke na kupenda utamaduni na bidhaa zao. Ina maana gani sisi kukimbilia kuvaa mavazi nusu uchi suruali zilizopasuliwa kila mahali na kuonyesha miili wakati tuna nguo bora zinazozalishwa hapa nchini?

Kuna haja yoyote ya kukimbilia mapambo ya plastiki kutoka dunia nyingine wakati kuna mapambo ya kupendeza yanayotengenezwa na vifuu vya nazi, manyoya ya ndege wa asili, bidhaa za ngozi na mifupa ya mifugo inayozalishwa Tanzania.

Mpinga unaotoka Tanzania unatengeneza vinyago bora vinavyopendeka dunia nzima na kutumiwa na makundi mbalimbali kuanzia mamilionea, matajiri wakubwa duniani na wafalme pia.

Watanzania ni vyema kuthamini vyakula vyetu kama ndizi nyama, kande, ugali, mboga kama mlenda, kisamvu na kitoweo kama samaki wa kukaushwa badala ya kujiendekeza kula chips muda wote.

Mara nyingi yameelezwa madhara ya kula vitu vya kukaanga kwa wingi ikiwa ni pamoja na kuongeza lehemu au mafuta ndani ya mishipa ya damu na ya moyo.

Yote hayo yanahatarisha afya na kusababisha matatizo ya figo, moyo, sukari na hata vifo iwapo kutakosekana tiba na uangalizi.

Kuna haja gani ya nchi kuagiza samani kutoka nje wakati iko mianzi inayoweza kutumiwa kuzalisha samani bora hata nyingine kuuzwa nje?

Karibuni Waziri wa Maliasili na Utalii Angela Kairuki, anatangaza mpango wa kuzalisha mianzi ambayo itatumiwa kusafisha hali ya hewa kwa kuondoa hewaukaa angani, lakini pia ikitengenezwa samani mbalimbali zinazoweza kuuzwa barani Asia.

HABARI KITAIFA

# Viwango vya riba kubadilisha fedha vinavyoathiri madeni nchi za Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

MADENI ya nchi nyingi za Afrika yanakua kwa kasi kutokana na kuongezeka kwa viwango vya riba na kubadilisha fedha duniani na kusababisha kushuka kwa thamani ya fedha za ndani. Imeelezwa.

Hayo yamebainishwa mjini Victoria Falls, Zimbabwe na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa Mkutano wa 56 wa Mawaziri wa Fedha, Mipango na Maendeleo ya Uchumi kutoka nchi za Umoja wa Afrika (AU) unaoratibiwa na Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa (UNECA).

Alisema awali ukuaji wa deni ulikuwa unaendana na ukopaji lakini kwa sasa imebainika kuwa kuna sababu zingine zinazochochea kuongezeka kwa deni hilo, ikiwa ni pamoja na mabadiliko makubwa ya viwango vya kubadilisha fedha na riba hivyo kuzifanya nchi za Afrika kutafuta njia mbadala ya kutatua changamoto hiyo.

Mwandumbya pia alisema katika kukabiliana na ukuaji wa madeni, hususani kipindi hiki cha mabadiliko ya tabianchi, ni lazima kwa Afrika kuwa na mkakati kuhakikisha zinapata rasilimali fedha ili mipango inayotekelezwa kukidhi mategemeo ya wananchi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana mawazo hasa kwenye kaulimbiu ya 'Financing the Transition to Inclusive Green Economies in Afrika' inayotoa hamasa na kutafakari njia ambazo zinaweza kutumika kufadhili uchumi na kufanya uwekezaji ambao unazingatia mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Kida alisema kwenye mkutano huo wameweza kuona njia nyingi mpya zinazoibuka za kusaidia uchumi hususani mikopo nafuu kwenye uchumi wa kijani, ambayo inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kufadhili mipango na miradi ya maendeleo.

Mkutano huo wa 56 unaoratibiwa na UNECA ni jukwaa ambalo limeanzishwa na Umoja wa Mataifa (UN) ili kuzisaidia nchi za Afrika kufanya mijadala na utafiti mbalimbali ili kuzalisha na kufanya ubunifu utakaokuza uchumi hivyo kutengeneza fursa ya kujadiliana na kuhakikisha ushauri unaotolewa unaendana na mazingira halisi.



Meneja Mwandamizi Huduma za Kidigitali wa Benki ya CRDB, Mangile Kibanda (kulia), akizungumza wakati wa kuchezesha droo ya kwanza ya msimu wa tatu wa kampeni ya 'Benki ni SimBanking', jijini Dar es Salaam jana, ambapo washindi watatu walipatikana wakiwamo wawili wa pikipiki moja kila mmoja na mwingine wa Bajaj. Kushoto ni Ofisa Masoko wa Benki hiyo, Salim Salim na Ofisa wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Clara Chacha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yaanika vikwazo ustawi wanawake

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, mwaka huu, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimebaini kuwa biashara nyingi za wanawake zinakwama kutokana na matatizo ya kimfumo na miundombinu ikiwamo maji, umeme na barabara.

Aidha, imeiomba serikali kuanzia ngazi za manispaa, mitaa na vitongoji kutatua kero zinazokwamisha wanawake kushindwa kufikia malengo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, aliyabainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, iliyobeba kauli mbiu inayosema 'Wekeza kwa Wanawake Kuharakisha Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii'.

Pia alisema wamebaini wanawake wafanyabiashara hasa, masokoni na viwandani, wanakumbana na udhalilishaji wa kijinsia wanapotimiza majukumu yao.

"TAMWA tunamsherehekea mwanamke aliyethubutu, akatimiza na tunaikumbusha jamii kuendelea kuwapa ushirikiano wanawake wanapothubutu kujikwamua kiuchumi," alisema Dk. Reuben.

Alisema TAMWA imeamua kumsherehekea mwanamke shujaa kuanzia ngazi ya chini, ambaye anajishughulisha au amejiajiri katika eneo lolote ili kujitafutia riziki na kujikwamua kimaisha na ameweza kustahimili changamoto za ugumu wa maisha kama vile ukame unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi, ukosefu wa maji na kukatika kwa umeme na magonjwa ya mlipuko.

Dk. Reuben aliwataja wanawake hao ni wale walio katika makundi ya mafundi wa magari, wauza mboga, mama lishe, dereva bodaboda, mvuvi, mchimba madini, utingo wa mabasi, wanawake wafanya biashara kubwa na ndogo, wanasiasa na wale walio katika taasisi mbalimbali.

"Tunaamini katika usawa wa kijinsia maeneo yote, hivyo kwa mwanamke kuthubutu kufanya kazi na kustahimili maisha kwetu tunaona kathubutu. Kadhalika, TAMWA inawaadhimisha wanawake hawa kwa uthubutu wao ili wawe mfano kwa wengine ambao wanapitia unyanyasaji kwa kukosa kipato au kudhani hawawezi.

"Mwaka huu mwanamke aliyeamua kujishughulisha katika kazi au biashara halali inayomwingizia kipato ni shujaa kwetu na ndiyo maana kauli mbiu yetu sisi TAMWA mwaka huu tunasema; 'Kathubutu Katimiza'," alisema.

Dk. Reuben alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuthubutu na kutimiza kuendelea kutengeneza mazingira wezeshi kwa wanawake.

"Uamuzi wake wa masuala ya kisera na kimkakati kupitia falsafa yake ya 4R ndiyo yanayofanya wanawake katika sekta mbalimbli zikiwamo na asasi za kiraia kufanya vizuri katika maeneo maeneo mbalimbali. Jambo ambalo litaendelea sasa kuonyesha umahiri wao utakaomrahisishia kuongeza teuzi za wanawake katika uongozi na ngazi za juu za maamuzi," alisisitiza.

Mwakalishi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Vera Assenga, alisema wanashirikiana na TAMWA katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kuwaelezea wanawake wanaofanya mambo makubwa ndani ya jamii lakini hawajapewa nafasi ya kutambuliwa.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



# Waziri atuliza mgogoro uwekezaji mashamba

**Na Munir Shemweta,** BABATI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewatuliza wananchi wa vijiji vya Kimara na Kiru Dick, Babati mkoani Manyara kutokana na mgogoro na wawekezaji wa mashamba.

Hatua hiyo inatokana na wananchi wa vijiji hivyo kuingia kwenye mgogoro mkubwa na wamiliki wa mashamba ya Miombo Estate na Hamir Estate yaliyoko Bonde la Kivu wilayani hapa. Uamuzi huo ni utekelezaji wa maagizo ya Katibu Mwenezi, Itikadi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ambaye katika ziara yake mkoani Manyara, aliwasilishiwa malalamiko kuhusu mgogoro huo na kumwelekeza Naibu Waziri Pinda kwenda kutafuta suluhu.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa vijiji hivyo juzi wilayani Babati akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Manyara, Pinda aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kushughulikia mgogoro huo.

"Kwa hiyo ninachokuja kuwaambia nyie, kwanza, ni utulivu na kitu kikubwa kitakachotutawala katika hili ni utulivu na kwa jinsi tunavyokwenda kukubaliana mnakwenda kupata maeneo mtakayokwenda kuendesha maisha yenu," alisema.

Aliwakumbusha wananchi wa vijii vilivyoingia kwenye mgogoro kuwa wasisahau kwamba uwapo wa wawekezaji kwenye maeneo hayo bado ni halali, hivyo wakati serikali ikiweka mambo sawa, basi waepuke ushabiki.

"Kwenye kipindi hiki ambacho tunakwenda kuyaweka mambo haya vizuri, ushabiki hautakiwi na lazima hekima iwatangulie. Tusipokuwa na hekima katika kutekeleza jambo hili, bado kutakuwa na mgongano ikiwamo kesi," alisema.

Kwa mujibu wa Pinda, ujio wake katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo wa mashamba wilayani Babati ni kusimamisha masuala ya kesi kwa zile pande zinazopingana ili kukaa meza moja na kumaliza mgogoro kwa lengo la wananchi kuishi kwa amani.

Awali, wananchi wa vijiji hivyo walimweleza Pinda kuwa wakati wa kutafuta suluhu ya mgogoro huo ahakikishe makubaliano makubwa ni makazi ya watu kutoguswa sambamba na wao kutambuliwa kwa kuwa wametokana na mababu zao waliokuwa wakiishi maeneo hayo.

"Tunashauri kwamba nyumba za watu katika mgogoro huu unaokwenda kutatuliwa ziangaliwe kwa busara. Tuangalie makazi ya watu yasiguswe na mgogoro huu tena," walisema.

Wananchi hao walimshukuru Naibu Waziri Pinda kwa kwenda katika vijiji hivyo kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Hivyo kutaka kumalizwa viziuri ili wananchi waishi vizuri na wawekezaji.

Wawekezaji wa mashamba ya Miombo na Hamir, walimweleza Pinda kuwa hawana nia mbaya na wananchi wa vijiji vinavyowazunguka na kueleza kuwa hata uamuzi wao wa kuachia sehemu ya maeneo ya mashamba wanayomiliki ni kutaka kuishi kwa amani na kuepuka ugomvi na wananchi.



Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (katikati), akimtambulisha Naibu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Nasib Mramba (kulia) kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alipokwenda kutoa vyeti kwa wahitimu wa kozi ya wahudumu wa kwenye mabasi ya abiria chuoni hapo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wazalishaji wafundwa usalama chakula

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewakumbusha wazalishaji wa chakula kuimarisha mfumo wa usimamizi wa usalama wa chakula ili kulinda afya ya jamii na kudumisha imani ya walaji katika bidhaa wanazozalisha.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TBS, Prof. Othman Chande Othman, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku nne ya wakufunzi wa mfumo wa usimamizi wa usalama wa chakula yaliyoandaliwa kupitia viwango vya mradi endelevu.

Mafunzo hayo yalikutanisha washiriki kutoka Uganda, Kenya, Ethiopia, Somalia, Mauritius, India na Uswisi.

Prof. Othman alisema usalama wa chakula ni muhimu kwa kampuni za chakula kuhakikisha zinazingatia mahitaji ya udhibiti na kuongeza kuwa hiyo ni moja ya vipengele muhimu katika ajenda ya usalama wa chakula duniani.

"Kwa kutekeleza mpango wa usalama wa chakula, kampuni zinaweza kutambua, kuzuia na kushughulikia hatari zinazoweza kutokea kwa chakula, kupunguza hatari ya magonjwa yanayotokana na chakula na kuepuka uharibifu wa sifa ya kampuni zao," alisema Prof. Othman.

Alisema ni heshima kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mafunzo hayo ambayo yanalenga kuwapa ujuzi wataalamu wa Afrika katika sekta ya chakula kuhusu mahitaji na manufaa ya viwango vya usimamizi wa usalama wa chakula.

Mafunzo hayo, alisema yatasaidia mashirika ya viwango ya taifa kutoa huduma bora kwa jamii na shughuli za uhamasishaji kuhusu jukumu la viwango hivi katika kuchangia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG).

Alisema sekta ya chakula inakua kwa kasi kutokana na mahitaji na teknolojia hivyo usalama wa chakula ni suala la afya ya binadamu na vizazi vijavyo.

Pia aliongeza kuwa mafunzo hayo ni ya msingi kwa wote na aliishukuru sekretarieti ya Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO) kwa kutambua umuhimu wa kuboresha elimu ya viwango vya usimamizi wa usalama wa chakula ndani ya Kanda ya Afrika Mashariki.

Prof. Othman alisema nchi hizo zimechaguliwa kati ya nchi 11 wanachama wa ISO kutoka Afrika Mashariki na kwamba Shirika lao la Viwango la Taifa hufanya kama vituo vya mawasiliano na kwa upande wa Tanzania ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

"Napenda kumpongeza kila mmoja wenu kwa kufanya vyema katika mchakato wa uteuzi. Mashirika ya Kitaifa ya Viwango yamewakabidhi ninyi wakufunzi wajibu huu, wakiamini kwamba mnaweza kutoa kile kinachohitajika.

"Napenda kuwasihi mchukue fursa hii kwa kujitolea sana kwani mtatakiwa kuhamishia maarifa mliyopata kwa wenzako katika nchi zenu na bara zima kwa ujumla," alisisitiza.

Alisema baada ya siku hizo nne, washiriki wa mafunzo hayo wataendelea na mafunzo ya masafa kwa mashirika ya majaribio na hatimaye watapangwa tukio la kujenga uelewa pamoja na mashirika yao ya viwango kabla ya kumalizika kwa mradi unaotarajiwa kuwa Agosti mwaka huu.

Alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TBS na timu yake kwa juhudi zote walizofanya kuleta mafunzo hayo nchini Tanzania na kuongeza kuwa anaamini kuwa wataendeleza sifa ya nchi ambayo Tanzania inayo ya watu wakarimu na amani.

# Madereva, wahudumu wasisitizwa mafunzo

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) madereva na wahudumu wote wa usafiri wa umma kupatiwa mafunzo ya namna ya kutoa huduma ya kwanza ndani ya kipindi cha miaka mitatu.

Mafunzo hayo, yameelezwa kuwa ni muhimu kwa kuwa yatasaidia kuokoa maisha ya abiria inapotokea ajali kwa sababu madereva na wahudumu watakuwa na uwezo wa kuwapa abiria huduma ya kwanza.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alitoa agizo hilo wakati akifunga mafunzo na kutoa vyeti kwa wahudumu wa mabasi yaliyoendeshwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

"Naiagiza LATRA iwasilishe mpango mkakati serikalini wa namna ya kuhakikisha wahudumu wote wa mabasi na madereva wanapata mafunzo ya namna bora yaa kuwahudumia abiria wakati wa dharura ili tujue mwaka wa kwanza mtafanya nini hadi mwaka wa tatu mtafikia lengo gani," alisema.

Kihenzile alitoa wito pia kwa vyuo vingine kuiga mfano wa CBE kwa sababu mahitaji ya mafunzo ya aina hiyo ni makubwa na chuo hicho hakiwezi kutoa mafunzo kwa wahudumu wa mabasi yote yanayokadiriwa kufikia 5,000.

Aliipongeza CBE kwa ubunifu mkubwa wa mafunzo hayo ambayo alisema yamekuja wakati mwafaka kwani sekta ya usafiri itapata heshima.

"Kusema kila mtu anaweza kusema, kupanga kila mtu anaweza kupanga lakini kwenye utekelezaji watu wengi wanashindwa kutekeleza lakini hapa CBE mmekuwa mkipanga na mnatekeleza," alisema.

Alisema moja ya maeneo ambayo Watanzania wanalalamikiwa ni eneo la utoaji wa huduma na baadhi ya waajiri wanalazimika kwenda nje ya nchi kutafuta watumishi wa kufanya nao kazi.

Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga, alisema tangu waanze mafunzo hayo mapema mwaka huu, wameshatoa wahitimu 42.

Prof. Lwoga alisema sekta ya usafiri wa umma inakabiliwa na uvunjifu wa sheria na mmomonyoko wa maadili ndivyo sababu CBE iliamua kuanzisha mafunzo hayo ili kukabiliana na changamoto hizo kwenye usafiri wa umma nchini.

"Katika kuunga mkono juhudi za serikali tuliamua kuanzisha mtaaala huu mwaka jana na ukasajiliwa na LATRA kwa hiyo mafunzo haya yanatolewa kwa mujibu wa sheria ndiyo maana tunawahimiza wenye mabasi walete watumishi wao," alisema.

Alisema wahudumu hao wamejifunza kwa vitendo matumizi ya mifumo ya tiketi za kielektroniki na maadili wanayopaswa kuzingatia wakati wote wanapokuwa wakitoa huduma kwenye kazi zao.

# Mtanzania aliyewaongoza wamisionari kuhubiri injili afariki akiwa na miaka 113

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KIKONGWE Helena Seka, aliyekuwa miongoni mwa Watanzania watatu waliochaguliwa kuongozana na wamisionari wa Ujerumani waliokuja nchini kuhubiri injili mwaka 1911, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 113.

Huku akiwa ameacha uzao wa watu 415. Kati yao wamo watoto wake wa kuzaa saba, wajukuu 55, vitukuu 234, vilembwe 122, kilembwekezi mmoja. Marehemu Helena, aliyekuwa mkazi wa Ashira-Marangu, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, anatajwa kuwa mtu aliyekuwa na ushiriki wa moja kwa moja na wamisionari wa Leipzig waliozunguka Afrika kueneza dini.

Katika maziko yake yaliyofanyika juzi, yalikuwa kama sherehe kutokana na mamia ya waombolezaji kufurika wakiwa wamebeba maua, huku wakiimba na kusifu ukuu wa Mungu kwa umri mrefu zaidi kwa mtanzania huyo.

Akihubiri katika ibada hiyo iliyofanyika Usharika wa Masia Mshiri wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mch. Winford Mosha, ambaye ni Mkuu wa Jimbo Mstaafu la Kilimanjaro Mashariki alisema kikongwe huyo, ndiye aliyewaongoza wamisionari kutoka Kilimanjaro kwenda Ruruma-Singida kuhubiri injili kuanzia Desemba mwaka 1911.

Kikongwe huyo anadaiwa kwamba pia ndiye mtanzania wa kwanza kupona saratani ya matiti mwaka 1985 katika mazingira ambayo yaliwashangaza wengi.

# Asilimia 10 ya watoto wenye mtindio ubongo wanapelekwa hospitali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MTAALAMU wa afya kutoka Kituo cha Huduma za Utengamao kwa Watu Wenye Ulemavu kilichoko Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Neophita Lukiringi, amesema kwa sasa watoto wenye ulemavu wa mtindio wa ubongo wanaopelekwa hospitalini kupata matibabu ni asilimia 10 kati ya 75.

Idadi hiyo ni ya watoto wanaotumia vitimwendo visaidizi sahihi, kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Lukiringi, ambaye ni Mratibu wa Huduma za Vitimwendo wa kituo hicho, alikuwa akizungumza jijini Arusha jana, kuhusiana na matumizi sahihi ya viti mwendo.

"Kulingana na uzoefu tulionao wa kazi, asilimia 75 ya wateja wetu wakiwamo watoto wenye ulemavu wa mtindio wa ubongo na uchelewaji kwenye makuzi, wanaohitaji vifaa saidizi vya viti mwendo ni asilimia 10 ya wenye uwezo wa kuvipata kutokana na uchache na gharama kubwa za kununua,"alisema.

Alisema kuna umuhimu wa kutoa vifaa sahihi watu wenye ulemavu kwa kuwa vitawasaidia kuwa na ujasiri na kumwezesha kufanya shughuli zake za kila siku.

Vilevile, alisema vitimwendo sahihi vitawasaidia kundi hilo muhimu kwenye jamii kukaa vizuri, kuboresha afya na kumuepusha na ulemavu mwingine ambao unasababishwa na vifaa ambavyo sio sahihi.

Aidha, Longini Mtalo, Mtaalamu wa Viungo Tiba wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, alisema kuna tatizo la upungufu wa wataalamu na vitimwendo kwa wahusika kutokana na kuwepo kwa mahitaji mengi.

Pia alisema kuna changamoto kwa baadhi ya watu, mashirika na wanasiasa wamekuwa wakitoa vifaa hivyo saidizi pasipo kuwashirikisha wataalam ambao wangetumia nafasi zao kutoa ushauri wa kitaalamu.

Amarine Shayo kutoka Wizara ya Afya, alisema serikali imeandaa mpango mkakati saidizi, kwa watu wenye ulemavu, ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki (katikati), akikagua mabanda kwenye maadhimisho ya siku ya wanyamapori duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Manyara, juzi. Kushoto ni Mkuu wa wilaya ya Babati, Lazaro Twange. **PICHA: GIFT THADEY**

# Misaada yazidi kumiminika kwa waathirika maporomoko Hanang'

**Na Mwandishi Wetu**

MISAADA kwa waathirika wa maporomoko ya tope wilayani Hanang' inazidi kumiminika, hivi sasa vifaa vya ujenzi vya Sh. milioni 7.7 vimepokelewa.

Maporomoko hayo yalitokea Desemba 3 mwaka jana na kusababisha uhalibifu wa miundombinu, mali pamoja na maelfu ya wakazi wa mji wa Katesh kukosa sehemu ya kuishi. Msaada huo umetolewa juzi na Benki ya Biashara ya Mkombozi na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja. pamoja na rangi za nyumba za mafuta na maji, (primer, solvent, red oxide, black paint), roller brush na hand brush.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo mkoani Manyara Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Respige Kimati alisema benki yao ni ya wananchi, ipo mbele katika kuhakikisha inatoa huduma mbalimbali za kibenki.

Alisema katika nyakati kama hizo wamekuwa wakiungana na Watanzania kuwashika mkono kama walivyofanya kwa wananchi wa Hanang' kwa namna moja ama nyingine, kuwarudisha katika hali yao ya kawaida.

"Tunafurahi sana siku ya leo kukabidhi vifaa hivi kwa ofisi ya Mkuu wa Wilaya hii ya Hanang kama msaada wetu ili kwa utaratibu mliojiwekea uweze kuwafikia wale wote wananchi waliopata na maafa,"alisema.

Aliongeza: "Tunatoa pole kwa wale waliopatwa na maafa ambao walipoteza ndugu na jamaa zao, Benki ya Mkombozi inatazama na kushughulika na wateja wa aina zote, tumeweka kipaumbele kwa wateja wadogo wadogo wakiwemo wa vijijini na kujenga mtandao ambao utaimarisha utoaji wao wa huduma za kibenki"

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja alishukuru uongozi wa benki hiyo kwa kufika katika wilaya hiyo kwa kwenda kuwapa pole waathirika na kuwapatia vifaa vya ujenzi. Alisema takribani nyumba 108 zinatarajia kuanza kujengwa ndani ya wiki hii, huku miundombinu mbalimbali ikiwa imekamilika katika eneo hilo la ujenzi ikiwemo maji, umeme pamoja na miundombinu ya barabara.

"Tunashukuru Mkombozi Benki kwa kutukimbilia kwa upendo wenu, Hanang inaendelea kurudi katika hali yake ya awali hatua kwa hatua, hivyo vifaa hivi tulivyopokea lengo lake kubwa ni kuongeza nguvu katika ujenzi huu wa nyumba,"alisema.

Aidha aliwasihi uongozi wa benki hiyo kuangalia namna ya kuwagusa wakulima, wafanyabiashara katika kuwainua kiuchumi.

# TAWIRI yaanza matumizi ya teknolojia akili mnemba

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Nchini (TAWIRI), imeanza matumizi ya teknolojia ya akili mnemba, kufanya utafiti wa wanyamapori na kuchakata takwimu na uchambuzi wa picha zinazotokana na kazi ya kuhesabu wanyama hao.

Jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI, Dk. Eblate Mjingo akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, alisema teknolojia hiyo imerahisisha utafiti wa wanyamapori nchini kufanyika kwa wakati na kwa usahihi zaidi.

Alisema matumizi ya teknolojia hiyo kwa shughuli za uhifadhi wa wanyamapori yana tija kubwa katika uhifadhi endelevu.

"Miongoni mwa teknolojia zinazotumika katika utafiti wa wanyamapori hivi sasa ni pamoja na matumizi ya artificial intelligence (akili mnemba) kwa ajili ya kuchakata takwimu na uchambuzi wa picha za sensa ya wanyama.


"Lakini pia, tunatumia vilevile, teknolojia ya GPS satellite Collar (mikanda ya visukuma mawimbi), kufuatilia mienendo ya wanyamapori pamoja na matumizi ya ndege zisizo na rubani, kutatua changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu."

Mbali na teknolojia hizo, yamo matumizi ya helikopta/ndege za kuwafuatilia wanyamapori kwa ajili ya matibabu na kuwarejesha wanyamapori kwenye maeneo ya hifadhi.

Pamoja na mambo mengine, Dk. Mjingo, alisema TAWIRI hivi sasa inatumia kamera za kutega ili kubaini aina ya wanyamapori waliopo katika maeneo mbalimbali, changamoto za uhifadhi na kutumia chembechembe za vinasaba (DNA), kutambua afya ya uzazi wa wanyamapori kwenye mifumo ikolojia.

Wiki iliyopita, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki alisema serikali imepanga kuwekeza zaidi kuendeleza uhifadhi, kwa kujumuisha teknolojia za kisasa.

Kwa mujibu wa Waziri Kairuki, utekelezaji wa mpango wa matumizi ya teknolojia za kisasa katika uhifadhi, tayari viongozi wa Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Burunge, walipelekwa Ikona WMA kujifunza matumizi ya technolojia za kisasa kuzuia migogoro baina ya binaadamu na wanyamapori.



# RC aruhusu mafundi wenye leseni kukagua majengo

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MAFUNDI umeme waliosajiliwa na kupata leseni kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini (EWURA) wameruhusiwa kupata vibali vya kukagua miundombinu ya umeme kwenye majengo ya serikali.

Mafundi hao wamepewa ruhusa hiyo ili kuondoa adha ya kuwasubiri kwa muda mrefu wakaguzi kutoka Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).

Ruhusa hiyo imetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela wakati akizungumza na wadau wa sekta ya umeme kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuwaagiza TEMESA kuhakikisha wanatoa vibali kwa mafundi hao ili kurahisisha kazi.

Shigela alisema hatua hiyo itasaidia majengo ya serikali kukaguliwa na kufunguliwa mapema sanjari na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati badala ya kusubiri wakaguzi kutoka TEMESA ambao wamekuwa wakichelewa kufanya ukaguzi wa majengo hayo.

Alitolea mfano mkoa huo kuwa una zaidi ya vijiji 486, hivyo baadhi ya majengo ya serikali yanayojengwa na kuwekewa miundombinu ya umeme na makandarasi, mafundi yamekuwa yakichelewa kufunguliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kutokana na wakaguzi kutokufika kwa wakati.

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa Victoria, George Mhina alisema kanda hiyo ina mafundi umeme 1,108 waliosajiliwa na mamlaka hiyo Mkoa wa Mwanza, ukiongoza kwa kuwa na mafundi 476, Geita 181 na Kagera 162 na kusema ni kosa kisheria mafundi kufanya kazi hiyo bila kusajiwa.

Hivyo, aliwaonya mafundi vishoka kuacha tabia hiyo mara moja kwani kuendelea kufanya hivyo ni kinyume cha sheria, kuwataka kufuatilia leseni zinazotolewa kwa kuzingatia viwango vya elimu na kwamba vyeti vinavyotolewa ni kuanzia hatua ya kwanza mpaka hatua ya sita.

Akijibu suala la utolewaji wa vibali, Meneja TEMESA Mkoa wa Geita, Mahangaiko Ngoroma aliwataka mafundi waliosajiliwa na EWURA kupeleka nyaraka zao kwa wakala huo ili ziwasilishwe makao makuu ili kupata kibali cha kuwaruhusu kufanya kazi hiyo.

Meneja huyo pia alikiri kuzuia baadhi ya majengo ya serikali mkoani hapa baada ya kufanya ukaguzi na kubaibini kuwepo wa kasoro za kiufundi wa umeme na kushauri mafundi waliofanya kazi hiyo kufanya marekebisho hayo.



Shekhe wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Makusanya akiongoza dua ya kumuombea Rais mstaafu Hayati Ali Hassan Mwinyi ili apumzike kwa amani, wakati wa maombi yaliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme (wa tano kushoto), katika viwanja vya Sabasaba, Manispaa ya Shinyanga juzi na kuhudhuriwa na viongozi wa dini mbalimbali na wananchi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Kampuni ya madini yajitosa kuinua ufaulu shuleni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya dhahabu Barrick Bulyanhulu, imejitosa katika mpango wa kuinua ufaulu wa wanafunzi wa shule za serikali, kwa kuwajengea umahiri walimu juu ya mbinu sahihi za kufundishia.

Mpango huo umelenga kuzifikia shule zote za serikali katika Halmashauri za Nyang'hawale mkoani Geita na Msalala mkoani Shinyanga, kupita fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR).

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo kwa walimu 336 wa Halmashauri ya Msalala, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri hiyo, Seleko Ntobi alisema lengo ni kuboresha sekta ya elimu na kuleta tija na matokeo mazuri kwenye mitihani ya mwisho ya kidato cha pili na nne.

Alisema mafunzo haya yatatolewa na wakufunzi wabobezi kutoka Chuo cha Ualimu Shycom, wanaowawezesha walimu hao jinsi ya kufundisha mbinu za kuelewa masomo na kujibia mitihani.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Hamisi Katimba alisema baada ya mafunzo hayo halmashauri inatarajia kuona utofauti mkubwa wa ongezeko la ufaulu katika shule zote hususani katika masomo ya sanaa, lugha, hisabati na sayansi na kuwataka walimu hao kufanyakazi kwa kuzingatia misingi na miongozo ya kazi zao.

Mwakilishi wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu, William Chungu alisema wataendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha maisha ya wananchi hususani katika sekta za elimu, kilimo na afya kwa kuhakikisha wanasogeza huduma karibu za jamii na kuwataka wananchi kuitunza miradi inayoanzishwa.

# DC: Marufuku kurekodi watoto wakifanyiwa ukatili

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, amepiga marufuku vitendo vya baadhi ya wazazi kurekodi video za watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, kisha kuzisambaza katika mitandao ya kijamii.

Amewataka kutumia nafasi hiyo kukemea ukatili huo ili kulinda utu wa mtoto husika.

Alitoa marufuku hiyo juzi kwenye Kongamano la Mwaka la Muunganiko wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali mkoani Shinyanga, lililolenga kutafakari mafanikio na utekelezaji wa shughuli za kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa mwaka 2023. Alisema mtindo wa maisha ya kisasa umewaathiri wazazi wengi na hata kusahau malezi bora ya watoto wao, huku wengine wakikuta mtoto wa jirani akifanyiwa ukatili hawakemei kitendo hicho bali wanafurahi na kuanza kurekodi video kwa kutumia simu zao na kuirusha kwenye mitandao ya kijamii.

"Kurekodi video hizo pia ni sehemu ya ukatili acheni, hebu rudini zama za zamani tuwe na malezi bora ya watoto, pamoja na kumchukulia mtoto wa jirani ni mtoto wako, ukimkuta anafanyiwa ukatili kemea ikishindikana chukua hatua za kisheria," alisema Samizi.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kuunga mkono mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kufanya nayo kazi ya kupinga ukatili wa kijinsia zikiwamo mimba na ndoa za utotoni ili jamii ibaki kuwa salama na kwamba shirika lolote litakapopata changamoto wasisite kuwasiliana naye ili waitatue.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omary, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yamesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukatili ndani ya jamii zikiwamo mimba na ndoa za utotoni na kwamba kwa mwaka jana hakuna ndoa hata moja ya utotoni ambayo ilifungwa wilayani hapa.

Mwakilishi wa dawati la jinsia kutoka Jeshi la Polisi Shinyanga, Takelove Ayo, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakifanya kazi kubwa na hata kuisaidia polisi katika kesi za ukatili ambapo zinakwenda kwenye dawati hilo zikiwa zimekamilika.

Naye Mwenyeki wa muunganiko wa mashirika hayo, Jonathan Manyama, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2021 na sasa kuna wanachama 36 na lengo lake ni kuunganisha nguvu na kuwa na sauti ya pamoja katika mapambano ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema: "Mkoa wa Shinyanga tulikuwa wa kwanza kwenye masuala ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto lakini sasa hivi ukatili umepungua na tupo nafasi ya 10 siyo namba moja tena".




Ukurasa 12

BURIANI MZEE MWINYI

**Kiongozi asiyeogopa vyombo vya habari**





Ukurasa 13

Rushwa, dhuluma zinavyokwamisha kushiriki na kushinda uchaguzi

siasa

JUMATANO MACHI 6, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**Dokta Asha Mahita akumbusha kuwekeza zaidi kwenye afya**



BURIANI MZEE MWINYI

# Huruma yake ilivyoingiza chai maharage barabarani

• Mwanzo ujio daladala, mabasi binafsi kumiliki usafirishaji

**Na Rahma Suleimani**, ZANZIBAR

UNAPOKUWA kiongozi mkuu unatakiwa kuzijua shida za wananchi na kufanya kila mbinu kuzitatua.

Ukiona mamia ya waliokupigia kura wanasimama juani muda mrefu au kutumia saa kadhaa kutembea wakinyeshewa na mvua barabarani, kisa hakuna usafiri, pasua kichwa utatue kero hiyo.

Ndicho alichofanya Mzee Ali Hassan Mwinyi, rais wa awamu ya pili, baada ya kuona usafiri ni shida mijini na vijijini, watu hawana huduma hiyo, akaamua malori ya mizigo mfano ya mchanga, mbao bidhaa za sokoni yatumike kusafirisha abiria mijini.

Ukawa ndiyo ujio wa usafiri uliopewa jina la 'chai maharage' jijini Dar es Salaam, kutokana na muundo wa kuweka viti au kupanga mabenchi kulia, kushoto na hata nyuma ya dereva ili abiria wakae, ikionekana kama watu walioko mezani.

Akitoa ushuhuda wa ujio wa usafiri huo, Hamad Rashid Muhammed, anasema:"Niwape mfano hai Mzee Mwinyi akiwa rais, nilikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, aliniita akasisitiza watu wapate usafiri . Wakati huo ulikuwa ni wa shida mno. Akaniuliza hivi hatuwezi kuruhusu malori ya mizigo kuchukuwa watu tukawasaidia? Nikamwambia sheria hairuhusu, labda tufumbe macho."




Chai maharage, daladala alizoruhusu Mzee Mwinyi. **PICHA: MTANDAO**

Hamad Rashid ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ADC, akikianzisha baada ya kuhama CCM, anasema hilo pekee linatosha kueleza ni kwa kiasi gani Mzee Mwinyi, alijali matatizo ya watu, na magari hayo yakaanza kusafirisha watu Bara na Visiwani.

Chai maharage au malori hayo yaliingia barabarani kutokana na kampuni ya mabasi hasa mkoani Dar es Salaam UDA kusuasua.

Baada ya kuruhusu chai maharage kampuni binafsi za wasafirishaji ziliingiza magari yao na kuanza kusarisha abiria Tanzania nzima na sekta hiyo sasa iko mikononi mwao.

Anasema Mzee Mwinyi alikuta matatizo chungu nzima -kukosekana nguo, viatu, mafuta ya kula, bidhaa muhimu na yote aliyatatua na maisha yakaendelea.

Aidha, anasema katika uongozi wake Tanzania iligomewa kupata misaada na taasisi za kimataifa, lakini akafanya mazungumzo na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia nchi ikafunguka katika masuala biashara, uchumi na fedha.

"Mzee Mwinyi alikuwa mvumilivu mno nakumbuka wakati fulani alitupiwa madongo na kulaumiwa mno. Wengine tulijaribu kujibu, alikaa kimya, akisema baba nashukuru mmenijibia kidogo. Hili ni suala moja la kumsifia. Alivumilia mengi,"anasema Hamad Rashid.

"Kubwa alilolifanya ni utu, uvumilivu, kupambana na rushwa kadri ya uwezo wake na kuruhusu sekta binafsi kufanya kazi, vyombo vya habari kutimiza wajibu wake na vyama vya siasa kuendeleza siasa  za ushindani bila ya matatizo yoyote,"anaongeza.

**HAJUI KISASI**

Hamad Rashid, anamsifu marehemu Mzee Mwinyi, kuwa alipenda kushauriana ili kufikia maamuzi ya pamoja. Hakuwa mtu wa kuamua jambo pekee na kuwataka viongozi na Watanzania kujifunza hilo.

"Kubwa jingine hakuwa na adui mkikosana hana tabia ya kuweka jambo rohoni, likimalizika anaendelea na ukurasa mwingine ikiwamo kuwa marafiki." Anaongeza.

"Watanzania watamkumbuka kwa mambo mengi likiwamo kuacha kujilimbikizia mali badala yake alitaka wananchi wapate fursa na hili ni la kuliendeleza katika nchi yetu kwa sababu maskini ni wengi kuliko matajiri, tukumbuke."anasema.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, Muhammed Aboud, anasema licha ya Mzee Mwinyi kuwa kiongozi na Baba wa Taifa, wakati wote alitumia elimu yake kuwafunza viongozi wake.

**INAENDELEA UK. 12**



# Kiongozi asiyeogopa vyombo vya habari




**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

NIUNGANE na Watanzania wote kuomboleza kifo cha rais mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi (98), aliyeongoza serikali ya awamu ya pili.

Mpendwa wa Watanzania alifariki Alhamisi iliyopita na kuzikwa Zanzibar kijijini kwake Mangapwani mwishoni mwa wiki.

Mzee Mwinyi licha ya kwamba amefariki anabaki kuwa hazina kubwa kwa taifa kutokana na mambo mengi aliyoyafanya enzi za utumishi wake, aliyeshika nyadhifa mbalimbali kuanzia ualimu, ubalozi, Rais wa Zanzibar na baadaye kuongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Itakumbukwa kuwa amefanya juhudi kubwa kuinua uchumi wa nchi kwani wakati alipoingia madarakani, hali ya uchumi ilikuwa ni mbaya ikihitaji mikakati madhubuti ya kuinua uchumi na hali za wananchi. Kazi kubwa aliyoifanya inampa sifa ya kuitwa "baba wa mageuzi ya kiuchumi."

Aidha, kwa kuwa moja ya jukumu kubwa la serikali ni kuwahudumia wananchi kwa kuhakikisha inaweka mikakati, mipango na mazingira wezeshi ya kuwaletea na kuwainua kimaendeleo kwa mtu mmoja mmoja na ya nchi alifanya makubwa kwenye siasa, jamii na uchumi.

> Ni hatua zilizochukuliwa kwenye Azimio la Zanzibar, lililotangaza rasmi kuachana na Azimio la Arusha na kuiondoa serikali kwenye biashara na uzalishaji viwandani na kutoa huduma.

Kwa ujumla haikuwa lelemama, ni kazi nzito yenye kuhitaji kuunganisha nguvu ya pamoja ili kufanikisha azma hiyo.

Mzee Mwinyi baada ya kuchaguliwa kuwa rais mwaka 1985 aliikuta nchi katika mazingira magumu ya kiuchumi. Changamoto za wakati huo alizokumbana nazo ni pamoja na athari za vita ya Tanzania na Uganda mwaka 1978-1979, kupanda bei ya mafuta duniani, mdororo wa uchumi duniani njaa na masharti magumu ya wahisani.

Hali ya watumishi wa umma na ofisi za serikali ilikuwa taabani, ofisi hazikuwa na maji, vyoo vilibomoka, vikichafuka kwa kukosa maji na usafi.

Milango na samani zilikuwa tatizo sugu na kwa ujumla alichofanya Mwinyi kubadilisha hali ya nchi alistahili sifa zote.

Kutokana na changamoto hizo Mwinyi alilazimika kufanya mabadiliko ya kisera na kisiasa ili kuchochea ukuaji wa uchumi na hatimaye kufikia azma ya serikali yake ya kukuza maendeleo ya nchi na kuongeza uhimilivu hata kama mambo yalikuwa magumu.

Kiongozi huyo ana sifa nyingi kama vile kuasisi sera ya ushirikiano wa sekta za umma na binafsi ( PPP), kwani katika kipindi cha uongozi wake, alitoa fursa ya ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa uchumi ambayo ilikuwa ni nafasi muhimu iliyoongeza wigo wa kuwaleta wananchi wote kujenga uchumi.

Msisitizo wa soko huria au uliberali ulipewa msukumo wa kipekee katika kipindi cha uongozi wake na sekta binafsi ikiruhusiwa kufanya biashara badala ya jukumu hilo kubaki kwa serikali chini ya mfumo wa ujamaa.

Ni hatua zilizochukuliwa kwenye Azimio la Zanzibar, lililotangaza rasmi kuachana na Azimio la Arusha na kuiondoa serikali kwenye biashara na uzalishaji viwandani na kutoa huduma.

Moja ya sababu iliyochangia Mzee Mwinyi kupewa jina la "Mzee wa Ruksa" ni uamuzi wake wa kutoa ruhusa na fursa kwa watu binafsi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi, jambo ambalo kwa miaka mingi halikufanyika na hivyo jukumu hilo kubaki kwa serikali pekee.

Kutokana na ugumu uliopo wa ujenzi wa nchi, ni muhimu sekta binafsi kushirikishwa moja kwa moja katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na uwekezaji ili kurahisisha kasi ya maendeleo.

Hivyo basi, uwekezaji binafsi aliubariki ukisaidia kuinua uchumi na kupunguza makali ya maisha kama vile uhaba wa chakula, nguo na mafuta na bidhaa zote muhimu.

Akizungumzia kazi za Mzee Mwinyi, mwanasiasa mkongwe Dk. Wilbrod Slaa, anasema: "Alipokuja na sera yake ya kufungua madirisha na milango, basi kila upepo uliingia vizuri na tukapata nafuu tofauti na ilivyokuwa kabla, ambapo hata dawa ya meno ilikuwa ngumu kuipata. Aliingia kipindi kigumu, akafanya kazi na Watanzania hawatamsahau kwa hilo na ndiyo maana wanamuita Mzee Ruksa."

"Ni ukweli kuwa ili kuongeza kasi ya maendeleo, ni lazima serikali iwe na fedha za kutosha za kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo na ile ya kimkakati. Kutokana na ugumu wa kufanya kila kitu pekee yake, ndipo umuhimu wa ushirikishaji wa watu binafsi na sekta hiyo unapoonekana." Anasema Dk. Slaa

Ndiyo maana Mzee Mwinyi aliishirikisha kikamilifu sekta binafsi ambayo ilichangia ongezeko la makusanyo ya mapato na hivyo kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi na hatimaye kufikia maendeleo ni katika kipindi chake cha uongozi ambapo uhuru wa vyombo vya habari ulitamalaki, tena vikiitwa muhimili wa wanne usio rasmi kutokana na umuhimu wake katika kuchagiza maendeleo." Anasema Dk. Slaa

Anasema watu binafsi waliruhusiwa kumiliki vyombo vya habari na uhuru wake ukawa chachu ya kuharakisha maendeleo kutokana na kuibua changamoto mbalimbali ambazo zililazimu serikali kuzifanyia kazi, anaeleza mwanasiasa huyo aliyewahi kugombea urais kupitia CHADEMA lakini pia akarudi CCM na kuwa kada na balozi Canada na baadaye Sweden lakini sasa amevuliwa hadhi hiyo.

Ni ukweli kuwa Mzee Mwinyi, amefungua njia na kuleta msukumo wa ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye uchumi, ambao umeendelea kuenziwa kwa vitendo na marais waliofuata baada yake hasa awamu ya tatu ya nne na sasa ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni wazi alilenga kuipunguzia serikali mzigo wa kuwahudumia wananchi na hivyo kuharakisha huduma muhimu za kijamii ili ziwafikie vijijini na mijini. Hakika Mzee Mwinyi utakumbukwa daima kwa kuweka misingi bora ya uchumi hasa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi na kuwafungua macho wajasiriamali na wafanyabiashara kote nchini.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0620 800 462.***

## Huruma yake ilivyoingiza chai maharage barabarani

**INATOKA UK. 11**

"Alituita kutukumbusha kufanya mambo ya kheri na bora na zaidi kuipenda nchi yetu, kwa hivyo msimamo wake wa mwanzo hakujali nafsi yake bali alisimamia maslahi taifa na watu,"anasema.

Anasema alipoanza uongozi wa juu alileta maridhiano na mabadiliko ya maendeleo, akianza na Zanzibar katika hali ngumu ya uchumi akamua kufanya uchumi huria ili maendeleo yapatikane.

Anakumbusha kuwa haikuwa rahisi kwa Tanzania Bara mambo yalikuwa magumu lakini aliyabadilisha kutokana na msimamo wake alifanya kazi kwa nguvu zake zote.

Mwaka 1984, Aboud anasema Mzee Mwinyi alipokuwa rais, Aboud alikuwa mfanyabiashara na kufunguka kwa biashara kutokana na miongozo yake kulimpa fursa ya kununua bidhaa nje ya nchi, akisema kabla ya Mwinyi biashara ilikuwa ngumu na maduka mengi yalifungwa Zanzibar.

Mwenyekiti wa CUF Professa Ibrahim Lipumba, anasema, alikuwa mshauri wa Mzee Mwinyi wa uchumi na anamkumbuka kwa mengi.

"Kulikuwa na machafuko ya kisiasa Zanzibar na wakati huo Rais alikuwa Aboud Jumbe(sasa marehemu) na Mzee Mwinyi akachaguliwa kuchukua nafasi yake. Haikuwa rahisi kuwaunganisha Wazanzibari lakini alimteua Maalim Seif Sharif Hamad (marehemu) Waziri Kiongozi.

Aliwaunganisha Wazanzibari wakawa shwari na kufunguka kwa uchumi watu wakitoka sehemu mbalimbali kufuata bidhaa Zanzibar." Anakumbusha Lipumba.

Anasema alipoanza kuongoza Tanzania mwaka 1985 nchi haikuwa na fedha za kigeni ,alifanya mabadiliko ya msingi ikiwemo kushusha thamani ya Shilingi.

"Atakumbukwa kwa ukarimu, busara, unyenyekevu, upole na kulinda haki za binadamu na mcha Mungu aliyeheshimu dini zote akiwaunganisha Wazanzibari na Watanzania katika kipindi chote cha uongozi," anasema Lipumba.

# Rushwa, dhuluma zinavyokwamisha kushiriki na kushinda uchaguzi

**Na Salome Kitomari**

KUKOSEKANA usawa wa kijinsia kunaendelea kuzua matatizo mengi kwenye chaguzi zinazofanyika na kusababisha wanawake kushindwa kugombea nafasi za uongozi kwenye serikali za mitaa, udiwani, ubunge na urais.

Baadhi ya wanawake washiriki wa uchaguzi mkuu na wa serikali za mitaa wanaeleza na kutaja madhila mengi yanayowakumba wakigusia kuombwa fedha, vitu na rushwa ya ngono.

Aidha, wanasema upo udhalilishaji, kuambiwa nafasi ni kwa ajili ya wanaume na kutoaminiwa na jamii zao, wakisema yote yameunguza ushiriki wao kwenye siasa

Mmoja wa waliogombea akisema kero ya kuombwa fedha, vitu na ngono imekithiri jambo lililomlazimisha kuuza gari lake ili kusaka uongozi, lakini juhudi zake hazikuwa na tija baada ya kuambulia patupu.

Hayo, yanaelezwa wakati wa kongamano la siku ya wanawake linaloandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Washiriki wa kongamano hilo wanataka vyama kuharakisha maboresho ya sheria kujumuisha suala la jinsia huku wakipongeza Sheria za Uchaguzi kuzuia udhalilishaji wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Mwenyekiti wa Wanawake TLP, Nuru Athumani, ndiye anayezungumzia kudhalilishwa na kuombwa rushwa ya ngono kuwa vimekithiri na kuwakwamisha kinamama kwenye uongozi.

Prisca Ngwesheni, aliyegombea udiwani kata ya Kitunda Dar es Salaam, anaeleza kuombwa rushwa ya fedha na ngono, lakini kuzuiliwa kwenye mikutano ya mitaa na jina kukatwa kwenye vikao vya juu kwa sababu hakutoa kitu kwa wajumbe, ni vikwazo pia.

"Unapotangaza nia uwe na fedha, kanga na madera kama huna fedha uchaguzi ni mgumu. Niliuza gari niliyopewa na mume wangu lakini fedha ziliisha sikuambulia kitu..." anashuhudia.

Mariam Machicha ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Machimbo Segerea, Dar es Salaam, anayeongeza vikwazo vingine akitaja kukosekana utayari wa kujitolea pamoja na kukosa fedha za kampeni ni tatizo kwa wanawake.

Lakini anawatia moyo kinamama akisema:"Wanawake wengi hukata tamaa, unatakiwa kutumia fedha zako kupata nafasi ya kujitolea. Wanaume wengi wanashinda uchguzi kwa sababu ya ujasiri hata kama hakuna posho. Ni wajanja ndiyo maana unasikia maeneo ya wazi yameuzwa na ukifuatilia wahusika ni wanaume." Anadai.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Machimbo, Mariam Machicha, akielezea vikwazo vinavyowazuia wanawake kwenye siasa. **Kulia;** mgombea udiwani kata ya Kitunda 2020, Prisca Ngweshemi (kulia), akimpongeza Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, wakati wa kongamano la wanawake. **PICHA: MWANDISHI WETU**

"Ni kipindi changu cha tatu lakini najitolea silipwi hata senti ni kazi ngumu lakini naifanya kwasababu naipenda," anasema Mariam.

Anataja takwimu za viongozi wanawake mkoa wa Dar es Salaam, akisema wenyeviti wa serikali za mitaa jumla ni 564, kati yao wanawake ni 64 tena wawili wanakaimu.

Anasema Manispaa ya Ubungo wenyeviti ni 90 na wanawake ni watano, Ilala ina 159 kinamama ni 28, wakati Temeke idadi yao ni 142 wanawake ni 12, Kigamboni ni 67 wanawake wapo wanne na Kinondoni wenyeviti ni 106 wanawake ni 18.

"Utakutana na ugumu wakati wa kuingia mara ya kwanza lakini ukiingia na kutekeleza wajibu wako watasema unatosha kama ilivyokuwa kwangu walisema ninatosha na kupigiwa kura zote, lakini ni muhimu sheria za vyama zikatoa nafasi kwa wanawake,"anasema.

## WAITAKA NEC

Mjumbe kutoka Mtaa wa Vijibweni, Vatherine Valence, anasema uongozi hao ni wa nafasi ya chini ila kuna majukumu makubwa na jamii haielewi kuwa shida zote za misiba, barabara, ugomvi wanandoa na migogoro ardhi zinaletwa kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa, wakati mwingine unashindwa kujigawa.

"Mwaka 2020 niligombea, jina likaondolewa kwa kigezo sijui kusoma na kuandika. Fikiria msomi na mhadhiri wa chuo kikuu bila kutaja (chuo chake) naondolewa eti sijui kusoma wala kuandika. Ndiyo maana tunasema uchaguzi wa serikali za mitaa usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na sio Waziri wa TAMISEMI."

"Huu ni uchaguzi muhimu kwasababu ndiyo wananchi waliko, ukiwa kiongozi ngazi hii unaishi na wananchi wa chini ni muhimu kufanya marekebisho,"anasema.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa CHADEMA, Susan Lyimo, anasema mwaka 2020 chama chake kiliweka wagombea 500 kwenye mitaa lakini walikatwa wakabaki 22 jambo ambalo haliwezekani "Tunachokisema ni kwamba mfumo ni mbovu, wanawake hawaonekani, inanishangaza kwa CCM kama tulijitoa wakabaki wenyewe iweje wanawake ni wachache hata CCM?"anahoji.

## UTAMBULISHO MAHSUSI

Aidha Suzan, anatoa angalizo, :"Ni lazima mfumo wa uchaguzi urekebishwe usimamiwe na NEC kwasababu ilivyo mtu anaweza kupiga kura zaidi ya mara mbili, akitoka mtaa huu kwenda mwingine hasa mijini kwasababu anaweza kujiorodhesha kwa majina tofauti na hakuna picha wala kufuatilia.

"Ni lazima kuwe na utambulisho mahusus wa mpigakura wa serikali za mitaa mtu apige picha mara moja kama ilivyo kwenye uchaguzi mkuu."

Kadhalika, anasema kwenye viti maalum uwakilishi umefika asilimia 40 na kutaka kwenye serikali za mitaa zilipo kazi kubwa kuwe na viti maalum.

Anasema viongozi wa serikali za mitaa na vijiji ndiyo wanaoshughulikia matatizo ya jamii walipwe posho au mishahara na akisema haiwezekani diwani ana posho, mbunge posho na mshahara na kwamba waliwahi kupendekeza bungeni posho za serikali na kupewa baiskeli kama mbunge anavyopata stahiki nono.

Kiongozi wa Kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Selemani Bishagazi anasema, ametembelewa na wanaume watiania mwaka huu na mwakani, lakini wanawake wataonekana dakika za mwisho, akiwaasa kujitokeza na kufahamiana na wajumbe.

Akiwasilisha ripoti ya uchaguzi wa serikali za mitaa, mtafiti Victoria Lihiru, kutoka Chuo Kikuu Huria, anasema kati ya wenyeviti wa vijiji 11,669 nchini wanawake ni 246 ikiwa ni asilimia 97.9 kwa 2.1, huku vitongoji ni 62,612 wanaume ni 58,441 na wanawake 4,171, kwenye mitaa 3,643 wanaume ni asilimia 67.4 na wanawake ni asilimia 12.6 pekee.

"Mwaka huu kutakuwa na ushindani mkubwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa wale waliokatwa 2020 watarudi kwa kasi kusaka nafasi zao, ni muhimu wanawake wakajipanga ili uwakilishi wao unaongezeke,"anasema.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya anasema ili kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye siasa na ngazi za maamuzi vyama vya siasa viweka kanuni na mifumo inayolenga kuwalinda wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia katika michato ya kisiasa na uchaguzi.

Aidha vitengeneza sera na mikakati yenye kulenga kuongeza ushiriki wa wanawake pamoja na makundi mengine katika siasa na uchaguzi wa sasa na mkuu 2025.

Taasisi za kusimamia chaguzi zihakikishe uwepo na utekelezaji wa kanuni zinazoweka mazingira bora yanayohamasisha ushiriki wa wanawake katika michakato ya siasa na uchaguzi.

Anawataka viongozi wa dini kuhamasisha wananchi wote ikiwemo wanawake, vijana na makundi mengine kusimamia haki yao ya kuchagua na kuchaguliwa kuwa viongozi katika nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi.

> Unapotangaza nia uwe na fedha, kanga na madera kama huna fedha uchaguzi ni mgumu.Niliuza gari niliyopewa na mume wangu lakini fedha ziliisha sikuambulia kitu...

KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE

# Dokta Asha Mahita akumbusha kuwekeza zaidi kwenye afya

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI na wanaharakati wanawake wamehamasisha jamii na kutoa ushahidi wa mambo mbalimbali kuhusu mafanikio na changamoto za wanawake kwenye uchumi, siasa, mila na desturi na fursa zilizopo kwenye dunia ya kidijitali.

Wanawake leo tutege masikio na kufungua macho, tujitazame ndani ya miili na roho zetu kwa kuadhimisha siku hii tukiangalia afya zetu na familia tunayoipenda, ni ujumbe wa Dk. Asha Mahita, kutoka Wizara ya Afya.

Akizungumza na Nipashe na kutoa ujumbe kwa wanawake mwaka huu, anasema: "Natamani mwanamke anapoadhimisha siku yake mwaka huu ajali na kulinda afya yake kwa sababu ataadhimisha kama ana afya nzuri lakini kama yuko kitandani hataweza kutoka.

"Natamani kila mwanamke alinde afya yake kwa sababu ataweza kutafuta kipato chake, kuhudumia vyema familia yake na atafanya majukumu yake kikamilifu. Tukumbuke afya ndiyo mtaji mkubwa kwa kila kitu," anakumbusha.

"Tujitafakari kama leo ni siku ya mwanamke duniani na utakwenda kwenye kongamano, kwanini usitumie muda huu pia kufika kituo cha afya kufanyiwa uchunguzi wa afya yako? Cha kwanza ni afya. Jiulize nitautumiaje muda wangu kutunza afya yangu?" anaeleza Dk. Asha anayeratibu matibabu ya wagonjwa wa nje ya nchi Wizara ya Afya.

Anashauri wanawake kwenda pia vituoni kufanyiwa uchunguzi wa afya wa maradhi kama saratani ya matiti, ya shingo ya kizazi, shinikizo la damu na kama wajijengee utaratibu wa kuchunguza afya kila wakati.

Anashauri kujenga mazoea kufanyiwa uchunguzi kila wakati au kutumia siku ya wanawake duniani au siku moja katika wiki hiyo inayoangukia Machi 08, kwenda kuchunguzwa afya kwa sababu dunia ya sasa imejaa magonjwa yasiyoambukiza mfano saratani, kisukari, figo, moyo, shinikizo la damu na matatizo ya mifupa.

Anawakumbusha wanawake kuwa utafiti unaonyesha kwamba maradhi hayo yakichunguzwa na kugundulika katika hatua za awali, matibabu yake yanaweza kuwa rahisi kuliko yakiachwa na kukomaa.

Anakumbusha kuwa kuna mengi ya kufanya ili kulinda afya mfano mwanamke na mazoezi, kuacha tabia za kubweteka, kuzingatia masharti yanayohusu ulaji bora na pia kuwatunza watoto, kuwapa chanjo zinazotolewa, akirejea kuzingatia kampeni inayoendelea ya chanjo ya surua na rubella.



Mratibu wa Wagonjwa Waotibiwa Nje ya Nchi na Tiba Utalii, Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> MEWATA tutashirikiana na Mamlaka ya Bandari hapa Dar es Salaam kuwapa elimu ya afya na kuwafanyia uchunguzi wanawake bandarini.

"Mwanamke na kuthamini afya ni pamoja na kutafuta na kusoma taarifa za afya kwenye magazeti, mitandaoni, majarida, kusikiliza wataalamu na vipindi vya redio na runinga na kuhakikisha kuwa unajali na kutunza afya yako," anaeleza Dk.Asha ambaye pia anaratibu Huduma ya Tiba Utalii katika Wizara ya Afya.

Anawahimiza kuwa magonjwa yasiyoambukiza ni pamoja na saratani, figo, moyo, kisukari, shinikizo la damu, changamoto za mifupa na kwamba ni vyema kujua hali zao ili kuwa na maisha bora na yenye afya.

Anafafanua kuwa kupitia kusoma na kutafuta taarifa za kiafya wataweza kujua pia habari za magonjwa mbalimbali kama yanayoambukizwa na virusi ambayo nayo pia ni tatizo la kiafya akitoa mfano wa homa ya ini na jinsi, kujikinga na kuzuia.

## HAMASA KWA MABINTI

Daktari huyu ambaye pia amekuwa mtumishi wa umma kwa miaka 20, anawapa nasaha wanafunzi wasichana walioko shuleni kujibidiisha kwenye kusoma sayansi ili taifa liwe na wataalamu wengi hasa wanawake katika nyanja mbalimbali.

Anaeleza kuwa wanawake na wanaume wana haki ya kupata elimu lakini ugumu kwa wasichana unakuwa pale wanaposema: "Mimi hiki kitu sikiwezi, kwa hiyo wanakosa uthubutu. Hayo tuyaache wewe mwanafunzi wa kike kuwa na uthubutu na kujiamini kuwa lazima nitajifunza sayansi na nitaweza." anahimiza.

Anaeleza kuwa kwa kusoma masomo hayo taifa litakuwa na wanawake wahandisi, madaktari wabobezi, watafiti na wabunifu kwa wavumbuzi kwa sababu Tanzania inawahitaji wasomi wa aina mbalimbali.

"Wanawake wakiamua kufanya kitu wanafanya kweli na wana uthubutu. Mfano tunao ni Rais Samia Suluhu Hassan, ni shujaa wa mambo mengi, tunaweza kama anavyoonyesha kikubwa ni kuwa na uthubutu kama yeye. Na kama Rais asingekuwa na uthubutu asingefanya hayo yanayoonekana," anasema na kuwataka wajifunze sayansi ili kuwe na wataalamu wengi wanawake kitaifa na kimataifa.

## KUSHIKAMANA KIMAENDELEO

Dokta Asha ambaye amekuwa Mganga Mkuu wa Hospitali mbalimbali kuanzia Temeke, Ilala na Jiji la Tanga, anawataka wanawake walio kwenye nafasi za kiuongozi, ngazi mbalimbali na hata utumishi wa umma kuwapa moyo na kuwashauri kikamilifu wanawake chipukizi na wanaoinukia ili waamue kubadilika na kuwa chachu ya maendeleo yao, familia na taifa.

Akizungumzia jinsi Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke 2024, yatakavyoakisi afya, anasema ni mwanachama wa Chama cha Madaktari Tanzania (MEWATA) na wameandaa upimaji wa afya kwa jamii ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha jamii kuthamini afya.

Dk. Asha Mratibu wa Masuala ya Jamii MEWATA, anasema kesho kutwa watakuwa maeneo mbalimbali kuhudumia afya za wanawake, kuanzia kuwapa elimu na kuwafanyia uchunguzi.

Mathalani, anasema kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kigamboni Dar es Salaam watafanya uchunguzi wa kiafya kwa wanawake.

Aidha, watashirikiana na wanaharakati wanawake Women Tapo kuwafanyia uchunguzi wa kiafya wanawake wajasiriamali wadogo wadogo kwenye kliniki itakayofanyika Mnazimmoja Dar es Salaam.

"MEWATA tutashirikiana na Mamlaka ya Bandari hapa Dar es Salaam kuwapa elimu ya afya na kuwafanyia uchunguzi wanawake bandarini,"anasema na kuwahimiza kinamama kujitokeza kupata huduma muhimu.

Anaeleza kuwa pamoja na kuwapa elimu ya afya kuhusu masuala mbalimbali mfano kuwachunguza matiti, shingo ya kizazi, presha, kisukari uzito mkubwa na matatizo mengine watakayoibua wanawake na pia wataalamu watakayokutana nayo.

Maadhimisho ya siku ya wanawake duniani mwaka huu yanaongozwa na kaulimbiu ya '

***Kaulimbiu ya mwaka huu 'Wekeza kwa wanawake kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii.'***



## Wafanyabiashara 15 kortini tuhuma ulanguzi bei ya sukari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA 15 waliokamatwa na Bodi ya Sukari kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi jijini kwa kulangua bei ya sukari wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, kusomewa shtaka la kuuza sukari kinyume na bei elekezi iliyotangazwa na serikali.

Wafanyabiashara hao walikamatwa baada ya kufanyika kwa msako wa kudhibiti walanguzi wa sukari katika maduka ya jumla na rejareja mkoani hapa, kwamba walibainika kuuza bidhaa hiyo bei juu kinyume na bei elekezi iliyowekwa na serikali ambayo ni kati ya Sh.2,700 hadi 3,000.

Msako huo ulifanyika Februari 19, mwaka huu jijini hapa chini ya Jeshi la Polisi na Bodi ya Sukari Tanzania.

Kwa mujibu wa Ofisa Mwandamizi Bodi hiyo, Fahiri Achi alisema wafanyabiashara hao wamekaidi maelekezo ya serikali ya kuuza bidhaa hiyo kwa bei elekezi.

"Operesheni hii nchi nzima na hapa Dodoma tumebaini wafanyabiashara wasio waaminifu waliopandisha bei ya sukari na kuuza kinyume na bei elekezi watahojiwa na Jeshi la Polisi," alisema.

Alisema wafanyabishara hayo wanauza sukari ya kilo 50 kwa Sh.190,000 hadi 200,000 wakati bei elekezi ni Sh.140,000.

"Kwa kilo 25 za sukari wanauza kwa Sh.105,000 hadi 110,000 wakati bei elekezi ni Sh. 70,000 iliyotolewa na serikali kwenye Tangazo Namba 40 la Mwaka 2023, Bodi ilitoa maelekezo mahsusi ya kusimamia bei elekezi," alisema.

Aidha, alisema wamebaini katika msako huo sababu za kutokushuka bei ni kwamba wafanyabiashara wa jumla na wa kati wananunua sukari kutoka kwa wasambazaji wakubwa, wanaficha kwenye stoo na kugeuka kuwa wafanyabiashara wa rejareja.

"Tumeona wanaweka sukari kwenye mifuko ya kilo moja hadi tano ili wauze kwa kilo moja Sh.4,400 hadi 5,000 kitu ambacho ni mzigo kwa wananchi na serikali haitafumbia macho suala hili," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mmeona kuna mfanyabiashara yule mhindi amenunua kwa Gulamali kwa Sh.140,000 sukari kutoka India lakini yeye anauza Sh.190,000 kitu ambacho si sawa, bodi tutasimamia suala hili kuhakikisha wananchi wanauziwa kwa bei halali iliyotangazwa na serikali."

# Tanzania kinara ufikishaji huduma ya intaneti Afrika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imetajwa kuwa nchi ya kwanza Afrika kwa ufikishaji wa huduma ya intaneti kwa kasi kwenye nyumba na majengo, huku ikishika nafasi ya pili kwa usalama wa mitandao.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama nchini (ICTC), Dk. Nkundwe Mwasaga aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio, mipango na mikakati ya kukuza TEHAMA nchini.

Alisema kwa mujibu wa vipimo vya utayari wa nchi kuhusu mitandao ya mwaka 2023 inayoandaliwa na taasisi za Portulans na Shule ya Biashara ya Said katika Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza inaonesha Tanzania inashika nafasi ya kwanza kwenye ufikishaji wa huduma ya intaneti kwa kasi kwenye nyumba na majengo.

Aidha, alisema kupaa kwa Tanzania katika usalama wa mitandao kunatokana na taarifa za Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kupitia Global Cybersecurity Index ambayo Tanzania ni mjumbe wa Baraza Kuu la ITU.

Dk. Mwasaga alisema mafanikio hayo ni jitihada za ICTC katika kubuni, kukuza na kuendeleza kazi na programu bunifu za teknolojia.

"Tunajitahidi kutoa fursa kwa vijana kubuni kazi na programu mbalimbali za TEHAMA ili kuendeleza teknolojia hii na kuifanya Tanzania ya kidigitali," alisema.

Kadhalika, alisema, katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa kidigitali, serikali kupitia ICTC inaendelea na mpango wa kujenga vituo nane vya TEHAMA nchini ili kuhakikisha inasimamia nguzo tano ikiwamo kukuza vipaji bunifu katika TEHAMA na kupanua wigo kwa vijana kufanya ubunifu na kuuendeleza.

Alisema vituo hivyo vinatarajiwa kujengwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Tanga, Mwanza, Mbeya na Zanzibar.

"Huu ni mpango wa awali, lakini mkakati uliopo ni kujenga vituo katika mikoa yote na wilaya zote, ili wananchi waweze kuvitumia na kujifunza suala zima la teknolojia na vituo hivi vitajengwa katika maeneo ya shule ambavyo vitasaidia vijana nchini kuendelea kuibua vitu mbalimbali vinavyouhusiana na teknolojia pamoja na kuendeleza, ambapo vitakuwa na uwezo wa kuingiza watu 200 kwa wakati mmoja," alisema.

Hivyo, aliwaomba wadau mbalimbali kushirikiana katika kuanzisha vituo hivyo, lengo likiwa ni kukuza vipaji tofauti na kulinda kazi bunifu za kiteknolojia.

"Ujenzi wa vituo hivyo ni sehemu ya vipaumbele 13 vya ICTC ambavyo vina lengo la kuleta mapinduzi ya teknolojia na ubunifu nchini. Tunatarajia kuanzisha kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA na vituo vya majaribio vya ubunifuTehama katika wilaya 10," alisema.

Hata hivyo, alisema watafanya utafiti wa maendeleo ya TEHAMA nchini na kufanya tathmini ya kitaifa ya hatua za utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya TEHAMA.



Wakazi wa Mtaa Muungano, Kata ya Nkuhugu, jijini Dodoma, Balozi Chinga (kulia), akiwa na Rahama Matiri wakipanga viroba vya mchanga jana, ili kuzuia maji ya mvua yasiende kwenye makazi yao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Dk. Msonde asisitiza matumizi ya NeST kwa walimu, waganga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKATIBU tawala wa mikoa nchini wametakiwa kuhakikisha wakuu wa shule za msingi na sekondari na waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya wanapewa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Manunuzi (NeST) ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde kwenye mafunzo ya mfumo huo jijini hapa.

Alisema serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi za kutekeleza miradi katika ngazi ya msingi, hivyo makatibu hao, wakurugenzi wa halmashauri na wakuu wa idara ya halmashauri wanapaswa kuhakikisha wanafundisha kwa ukamilifu wale wote wanaotekeleza shughuli za manunuzi katika ngazi ya msingi wakiwamo wakuu wa shule na waganga wafawidhi.

"Mkifanya hivyo shughuli za manunuzi zitakwenda vizuri, thamani ya fedha itaonekana kwenye miradi na itakamilika kama vile ambavyo serikali inataka, hasa ikizingatia kuwa serikali inakusudia kupeleka fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika maeneo haya," alisema.

Pia aliwataka wataalamu wote watakaohusika katika mchakato wa manunuzi kuhakikisha wanazingatia matumizi ya mfumo huo ili kujiepusha na makosa ambayo yatawatia matatani.

Awali, Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Erick Kitali alisema idara yake itaendelea kuwekeza katika kuboresha na kubuni mifumo ambayo ni rafiki kwa matumizi kwa manufaa ya serikali na jamii kwa ujumla.

Naye, Meneja wa Mafunzo na Huduma za Ushauri kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Castor Komba, alisema imehakikisha inaboresha mfumo wa ununuzi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi.





# TUCTA yaiangukia serikali utatuzi kero zinazowasibu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VYAMA vya wafanyakazi Mkoa wa Njombe vimeiomba serikali kushughulikia kero zao ikiwamo kucheleweshewa mishahara, mafao na kiinua mgongo, pamoja na kumaliza mgogoro wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Walitoa maombi hayo kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, wakati wa kikao kilichofanyika mkoani hapa kilichowakutanisha viongozi wa vyama hivyo wakiwamo wa mashamba ya chai na walimu.

Walisema hali imekuwa mbaya hususani kwa wafanyakazi wa mashambani juu ya maslahi yao, kwani wamekuwa wakicheleweshewa mishahara kwa muda mrefu.

Baadhi ya wafanyakazi hao akiwamo, Anastazia Nyigo, Mohamed Saad na Njamasi Augustine walisema kero hizo zinawashushia molari ya utendaji kazi.

"Waajiri wanachelewesha sana mishahara wakati mwingine wanaruka miezi hata miwili wafanyakazi hawapati pesa na ukija mwezi wa tatu analipa mshahara wa mwezi wa Januari," alisema Anastazia Nyigo.

Naye Njamasi Augustine alisema tatizo la mikataba ambalo linasababisha kukosa huduma za afya katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ambao unawataka kuwa na mkataba wa miezi 12 na kuendelea.

Awali Mwenyekiti wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) Mkoa wa Njombe, Dk. Mashaka Kisulila, alisema wameendelea kupokea na kushughulikia kero za wafanyakazi wakati wote.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alikiri kupokea kero hizo, huku akiahidi kwenda kukutana na waajiri wa mashamba ya chai na wafanyakazi na kutoa ushauri kwa CWT kusuluhisha migogoro yao ya ndani kwanza.

"Siku ya Alhamisi saa tatu tutaondoka na Kamati ya Ulinzi na Usalama twende huko tukaangalie pia tutajaribu kuongea na watu wa kilimo, Bodi ya Chai nao waje ili tutatue hizi kero kwa pamoja," alisema Mtaka.

Alisema: "Hawa walimu tunajaribu kufikiria unamwajiri leo sasa yule mwalimu anakuja kwenye chama ambacho wanagombana hadharani wanasema hawa wamekula hela, wamepelekana mahakamani ni kumwambia Joseph Msalaba (Naibu Katibu Mkuu CWT Taifa) huku tulikotoka ugomvi umesababisha vyama viwili vizaliwe kwa mlengo ya chama chetu tuangalie ni yapi ya kwenda kwenye adhara," alisema.

Wakitolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali za wafanyakazi hao baadhi ya waajiri ambao ni wakurugenzi wa halmashauri za Mkoa wa Njombe walikishauri CWT kuchukua hatua dhidi ya migogoro yao.

"Ni wazi na dhahiri kwamba tunayoyasikia kuhusu CWT yanatuvunja moyo," alisema William Makufwe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratias, alisema wanashirikiana vizuri na wafanyakazi na hawawindani kwamba kunapokuwa na kero wanakaa mezani na kuyamaliza.




Mkurugenzi wa Ukuaji na Ujumuishaji Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania, Kennedy Komba (kulia), akimpongeza Mwenyekiti wa Mtandao wa Wanachama wanaotoa Huduma za Kifedha kupitia Teknolojia (TAFINA), Cynthia Ponela, baada ya kuuzindua rasmi mtandao huo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## Magereza wapanda miti ya matunda kulisha wafungwa

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

ASKARI magereza wa Gereza la Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, wamepanda miti ya mbao 2,300 lengo likiwa ni kuhudumia wafungwa.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Mkuu wa Gereza Wilaya ya Ludewa, Johannes Baitange, alisema miti ya matunda imelengwa kuhudumia wafungwa wanaokuwapo katika gereza hilo.

"Tumepanda miche ya maembe 400, miche 240 ya machungwa na miche 300 ya maparachichi kwa ajili ya lishe ya wafungwa wetu na maabusu," alisema Baitange.

Kwa upande wake Mkuu wa Magereza Mkoa wa Njombe, Rashid Mangala, alisema zoezi hilo ni mwendelezo wa agizo la Kamishna Jenerali wa Magereza, Mzee Ramadhan Nyamka la kutaka maeneo yote ya magereza kupandwa miti.

"Tayari maelekezo yametoka kwa Magereza hapa Tanzania kupanda miti katika kuhakikisha kwamba tunaunga mkono zoezi hili na Gereza la Wilaya ya Njombe wao tayari, kuna hekari 500 zitapandwa," alisema Mangala.

Naye Muhifadhi wa Misitu kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Ludewa, Ramadhani Said aliwapongeza Magereza kwa kuona umuhimu kwa kupanda miti katika maeneo yao.

"Mpaka sasa kwa msimu huu wa mvua jumla ya miche tuliyowapa ni 4,300 kwa maana ya mwaka jana Desemba walichukuwa miche takribani 2,000," alisema Said.

Kadhalika, Mangala alipata fursa ya kukagua maendeleo ya mashamba ya mahindi yanayomilikiwa na gereza hilo ambalo limekuwa likiongoza kwa kuzalisha zao hilo kwa wingi nchini na kuwa na shehena kubwa ya chakula inayopelekea kulisha magereza mengine.

# 'Wanawake msiwadharau wanaume zenu mkifanikiwa'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE wa Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe, wametakiwa kutowadharau na kuwanyanyasa wanaume zao pindi wanapoteuliwa ama kuchaguliwa kuwa viongozi na wanapofanikiwa kiuchumi, ili kukuza ustawi wa familia zao.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri Mji wa Makambako, Zuwena Ungele, wakati akizungumza na Nipashe kuelekea Siku ya Wanawake Duniani.

Ungele alisema licha ya wanawake kuwezeshwa bado hawatakiwa kuwanyanyasa wanaume zao pindi wanapofanikiwa kiuchumi.

Hata hivyo Ungele alisema licha ya wanawake kufanikiwa kiuchumi bado wanatakiwa kuwaheshimu wanaume zao kwa kutambua kuwa ni vichwa vya familia. "Kwenye suala la elimu, kwenye suala la kujikwamua kiuchumi, kwenye suala la kushiriki katika shughuli za uongozi kwa hiyo sio lazima umwambie mwanaume apike, hivyo afanye kwa mapenzi, kuna mgawanyo wa majukumu lakini haikuzuii wewe kumsaidia mke wako," alisema Ungele.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji Makambako, Vaileth Ngesi, aliitaka jamii kutambua kuwa jukumu la malezi ya watoto ni la wazazi wote wawili.

"Sisi tunatoa wito kwa wanaume kwamba suala la malezi katika familia ni suala la watu wote, mwanaume na mwanamke na yule mtoto akisikia neno kutoka kwa baba akisikia neno kutoka kwa mama kwa jinsi Mungu alivyotuumba baba anasauti yake na mama anasauti yake," alisema Ngesi. Ngesi alisema ili kutenda haki kwa mtoto ni kushirikiana kwenye malezi pamoja na kuepuka matendo ambayo hayastahili ikiwemo kipigo, ubakaji na mengine mabaya.

Baadhi ya wakazi wa mjini Makambako akiwemo Gerald Tweve alisema pamoja na mapambano yote ambayo yanafanyika kwa wanawake lakini hawajiamini.

"Vitu vingi vinafanyika kwa ajili ya kumwinua na kumkomboa mwanamke lakini hawajiamini kwa maana wanapata nafasi lakini wanaiadhibu familia kwa kudharau wanaume zao," alisema Tweve.





# Samia asisitiza upatikanaji haki nchi Jumuiya ya Madola

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezitaka nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola kuhakikisha kuwa maendeleo ya teknolojia duniani yanachochea na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa haraka katika mahakama za nchi hizo.

Alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na mfumo wa kidijitali haunufaishi sekta nyenginezo na kuacha nyuma sekta ya sheria na kwamba wanachi wengi katika nchi zinazounda jumuia hiyo wanahitaji kupatikana kwa haki na kwa haraka.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola usiku wa kuamkia jana visiwani Zanzibar.

Rais Samia alisema ni fursa muhimu kwa washiriki ambao wengi ni wanasheria kujadiliana namna ya kuimarisha huduma ya mahakama na kwamba ni sehemu ya maendeleo.

Dk. Samia alisema Tanzania imekuwa ikipiga hatua kubwa ambapo kuna mageuzi makubwa katika undeshaji wa Mahakama sambamba na kuanzisha kutoa msaada wa sheria kwa wananchi vijijini hadi mijini, ili kila muhitaji apate haki hiyo.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza na kusimamia teknolojia katika kutoa huduma za kisheria kupitia mifumo ya kidijitali na kwamba teknolojia zinaondoa matumizi ya makaratasi katika mifumo ya Mahakama na sehemu za utoaji wa haki", alisema Dk. Samia.

Katibu Mkuu wa Jumuia hiyo, Patricia Scotland alisema mkutano huo ambao unafanyika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania, una lengo na kutumia maendeleo ya teknolojia katika kuhakikisha wananchi wa nchi za jumuia hiyo hawana kikwazo katika kupata haki.

Alisema Rais Samia ametengeneza mahusiano mazuri baina ya Tanzania na nchi nyingine kama ambavyo mfano mzuri kwa Hayati Julius Nyerere ambaye alisaidia katika kukuza uchumi wa maendeleo yanahitaji nguvu na mshikamano.

Naye Waziri wa Katiba na Sheria, Pindi Chana alisema nchi nyingi za madola zinaweza kuiga mfano katika kupiga hatua za huduma za kimahakama na hasa kutoa msaada wa sheria kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, alisema mkutano huo utaongeza ufanisi kwa wadau wa sheria na utawala bora wa nchi wanachama wa umoja huo, hususan Zanzibar jambo litakaloongeza ufanisi katika upatiknaji wa haki kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mkutano huu unaendelea mpaka Machi 8 mwaka huu ambapo utafungwa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi.

Mkutano huu ambao unafanywa kila baada ya miaka miwili, unafanyika Afrika baada ya kupita miaka 10 na umewakusanya mawaziri wa sheria na watendaji wengine katika nchi hizo.



Mkuu wa Kitengo cha Mama, Baba na Mtoto katika Kituo cha Afya Medewell, Kibaha, mkoani Pwani, Fatina Mziray (kulia), akimpima kiwango cha shinikizo la damu mmoja wa wagonjwa waliofika kituoni hapo juzi, kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, mwaka huu, ambapo kituo hicho, kinatarajia kuendesha kambi rasmi ya matibabu ya bure kwa magonjwa mbalimbali ya wanawake, itakayofanyika Machi 6 hadi 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yaonya matumizi chupa za plastiki zilizotumika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAALAMU wa afya kutoka kitengo cha maradhi yasiyoambukiza Wizara ya Afya, Mwanaisha Abdulrahman Mwarabu amewataka wananchi kuacha kutumia chupa za plastiki ambazo zimeshatumika kwa kuhifadhia maji, ili kuepukana na madhara ya kiafya ikiwemo saratani. Akizungumza na Nipashe jana kuhusu magonjwa yasiyoambukiza, alisema jamii imekuwa na utamaduni wa kutumia chupa hizo kwa kuhifadhi vitu mbalimbali ikiwemo maziwa, urojo na juisi jambo ambalo ni hatari kiafya.

Alisema chupa hizo zinazohifadhiwa maji viwandani huwa na kemikali baada ya matumizi ya maji hayo kumalizika na siyo vyema kuzitumia kwa matumizi mingine.

"Chupa hizo ni hatari sana kwa afya zetu kwa sababu madhara yake husababisha saratani za aina mbalimbali na watu wamekuwa na utamaduni wa kuzitumia chupa zilizomaliza kutumika kuhifadhia maji" alisema Mwarabu.

Aidha alisema kasi ya magonjwa yasiyombukiza ni kubwa ikiwemo shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na saratani, hivyo ni vyema kuchukua juhudi za kudhibiti kasi ya maambbukizi ya ugonjwa huo.

Alisema miongoni mwa juhudi hizo ni ulaji wa chakula bora, ufanyaji wa mazoezi na kupunguza matumizi ya vyakula vyenye mafuta mengi, sukari na chumvi.

Naye Meneja wa kitengo cha maradhi yasiyoambukiza Zanzibar, Dk. Omar Muhammed Suleiman alisema maradhi yasiyoambukiza kwa Zanzibar yanachangiwa zaidi na vitu mbalimbali ikiwamo mlo usiofaa na watu kutofanya mazoezi.

Alisema Wazanzibari ni watumiaji wakubwa wa kiwango kikubwa cha chumvi katika chakula na kusababisha kuwa na wagonjwa wengi wenye shinikizo la damu na kula vyakula visivyozingatia viwango vya lishe bora ambao wengi hula vyakula mtaani.

Hivyo aliwashauri wananchi kutopinga nasaha za watalamu wa afya kuhusu ulaji wa vyakula salama kinachozingatia protini, wanga, vitamini, mafuta kiasi kidogo na utumiaji wa maji ili kuepukana na maradhi yasiyoambukiza.

# Madaktari: Tujenge tabia ya kupima afya mara kwa mara

**Na Rahma Suleiman**

JAMII imetakiwa kuwa na tabia ya kuchunguza afya zao mara kwa mara ili kugundua magonjwa nyemelezi na kupata tiba mapema.

Ushauri huo umetolewa na Rais wa Rotary Club ya Zanzibar Stone Town, Augustine Mwombeki wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kambi ya uchunguzi na matibabu bure kwa wananchi wa Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja iliyofanyika Shule ya Kiongoni.

Alisema endapo jamii itaendeleza utamaduni huo itasaidia kugundua maradhi katika hatua za awali na kupatiwa matibabu kwa muda stahiki.

Alisema uwepo wa kambi za uchunguzi na matibu vijijini kunahasisha na kushajihisha wananchi kujitokeza kuchunguza afya zao na kuishauri jamii kuchangamkia fursa za kambi hizo pale zinapotokezea.

Aidha alizitaka taasisi nyingine za serikali na binafsi kushirikiana kujizatiti kutoa huduma bora za afya kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuunga mkono kambi kama hizo kufanyika mara kwa mara vijijini, kwasababu ni wazito kwenda hospitalini na huishia kutumia dawa za mitishamba jambo ambalo linahatarisha afya zao.

Alisema kuwa kambi hiyo ni kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa maradhi mbalimbali kwa watoto, wazee na kinamama wapatao 1,500 ambapo wamejipanga kutoa huduma tofauti zikiwemo uchunguzi wa magonjwa ya meno, macho, ngozi, masikio, koo na pua, Virusi Vya Ukimwi (VVU) pamoja na magonjwa ya kina mama katika kijiji hicho.

Akizungumzia kuhusu taasisi hiyo alisema kuwa ni taasisi ya kimataifa yenye lengo la kusaidia na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii ikiwemo huduma za afya. Naye daktari kutoka hospitali ya Tawakal, Madvan Nestory Rwegasira aliitaka jamii kuchangamkia fursa za kambi za uchunguzi na matibabu zinapotokea na zinasaidia kujua magonjwa nyemelezi ambayo yatasababishwa magonjwa makuu.

Baadhi ya wananchi waliopatiwa matibabu, akiwemo Zulfat Muhaji mkazi wa Kiongoni na Ali Matata Haji mkazi wa Mtende waliishukuru taasisi hiyo kwa kuweka kambi ya uchunguzi na matibabu kijijini hapo jambo litalowasaidia kugundua hali za afya zao na kupatiwa matibabu.

Walisema jamii haina tabia ya kuchunguza afya zao kutokana na gharama, ambapo wameishukuru taasisi hiyo kwa kuweka kambi hiyo na kuwataka wananchi kujitokeza katika kambi kama hizo ili kupata fursa ya kujua afya zao na kupatiwa matibabu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**QUEEN PAUL MASSAWE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA "PASSPORT" YENYE USAJILI **TAE104010** YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/2436/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PAULO NYAGWASWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0386/ 0102** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI GEITA mwaka 1989. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/17612024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAIDI IBRAHIM MADIRISHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN DUALIS** yenye usajili namba **T 811 DYJ,** CHASSIS NAMBA **KJ10206675** na ENGINE NAMBA: **MR2020665.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/29313/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RICHARD JASTIN KISANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T 304 BHU,** CHASSIS NAMBA: **SR500020754** na ENGINE NAMBA: **357959909.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MOS/TR/RB/269/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 11035 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE MICHAEL GODFREY JUSTINE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY 1. SUZANA RAMADHANI 2. RICHARD ELIYA BUTU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 27th day of March 2024

Dated at Korogwe this 5th day of March 2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA**

**(JENGO LA WIZARA YA ARDHI – KIVUKONI)**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 315 YA MWAKA 2023**

**JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO.......MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SHARIFA OTHMAN KHALID......MJIBU MAOMBI NA.1**

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED......MJIBU MAOMBI .2**

**RAMADHANI JUMA FIKIRINI......MKIBU MAOMBI NA. 3**

**KUITWA SHAURINI**

**RAMADHANI JUMA FIKIRINI......POPOTE ULIPO**

**JULIUS CHIPALA NYAMAKWELO**

Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (jengo la wizara ya Ardhi – Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 19/03/2024. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani "counter affidavit" ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa . vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hamtatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 20 Mwezi Februari, Mwaka 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 157 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late AMOS MWAKIBINGA of Nyerere Street, Ntyuka Ward within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY HELENA MWANAKATWE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 3, 2024

Dated at Dodoma this 4 Day of 3, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA**
**(JENGO LA WIZARA YA ARDHI – KIVUKONI)**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 37 YA MWAKA 2024**

**ESMAIL PROPERTIES LIMITED....................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**M/S MSS LOGISTIC COMPANY LTD.......................MJIBU MAOMBI NA. 1**

**SEMI YUPH SEMI.........................................MJIBU MAOMBI NA. 2**

**KUITWA SHAURINI**

**M/S MSS LOGISTIC COMPANY LTD**
**SEMI YUPH SEMI................................................POPOTE MLIPO**

**ESMAIL PROPERTIES LIMITED**

Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (jengo la Wizara ya Ardhi Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kusikilizwa tarehe 25/03/2024 saa 3:00 Asubuhi. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani "counter affidavit"ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyotevinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hamtatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/ amri kutolewa.

Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 04 Mwezi Machi, Mwaka 2024.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and administration Cause No 3843 of 2024**

**In the matter of the estate of the late of the TIMOTHEO MGANGA MABENANGA Of Dodoma Urban Within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by BEATRICE TIMOTHEO MGANGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 1 day of 4, 2024

Dated at Dodoma this 28 day of 2, 2024

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# UN yaibua utata matukio ya ukatili wa kingono

**JERUSALEM,** Israel

TIMU ya Umoja wa Mataifa (UN) imeibua matukio ya kutisha ya ukatili wa kingono dhidi ya wanawake wakati wa vita kati ya Israel na Hamas, na kwamba vimekuwa vikitekelezwa katika maeneo yote tangu mgogoro huo uanze Oktoba 7, 2023.

Katika ripoti iliyotolewa na timu hiyo inaelezwa kuwa kuna sababu kubwa ya kuamini kwamba unyanyasaji wa kijinsia unaendelea, baada ya kupata taarifa ya wazi zinazoonesha kuwa mateka katika Ukanda wa Gaza walinyanyaswa kingono.

Timu hiyo inaeleza kuwa imepata sababu za kuamini kwamba migogoro inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia kama ubakaji uliotokea wakati wa shambulizi la kigaidi la Hamas huko Israel, ikieleza kuwa hayo ni matokeo ya uhakika zaidi ya shirika hilo kuhusu unyanyasaji wa kingono.

Timu hiyo iliyongozwa na Mjumbe maalum wa UN anayeshughulikia unyanyasaji wa kingono katika migogoro, Pramila Patten, inaeleza kuwa ilitembelea Israel kati ya Januari 29 hadi Februari 14 kwa ajili ya misheni iliyolenga kukusanya, kuchambua na kuthibitisha habari kuhusu unyanyasaji huo wa kingono unaohusiana na migogoro kati ya taifa hilo na Hamas.

Inaelezwa kuwa timu hiyo pia ilienda katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa na Israel, na kwamba wadau wanadai kuwa matendo ya kikatili na kudhalilisha yalitokea, ikiwa ni moja ya kuongezeka kwa matumizi ya aina mbalimbali za unyanyasaji wa kijinsia.

"Matendo hayo ni pamoja na upekuzi wa mwili, vitisho vya ubakaji na kukaa uchi kwa kulazimishwa kwa muda mrefu, kwa Wapalestina walioko kizuizini," imesema UN.

Patten anasisitiza kwamba ujumbe huo haukukusudia kuamuru uchunguzi, na kwamba timu hiyo ilifanya mikutano 33 na taasisi za Israel na kuwahoji watu 34 wakiwamo walionusurika na mashahidi wa shambulio la Oktoba 7, 2023 na kukagua picha za saa 50 baada ya mashambulizi hayo kutokea.

Anasema ujumbe huo haukuweza kukutana na waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia licha ya juhudi mbalimbali walizozifanya, na kwamba siku ya kwanza alitoa wito kwa walioathirika kujitokeza lakini walitaarifiwa kuwa wachache miongoni mwao walikuwa wakipata matibabu ya kiwewe na hawakuwa tayari kujitokeza.

**HAMAS YAKANUSHA**

Kutokana na madai hayo ofisi ya kisiasa ya Hamas kupitia ujumbe iliyotoa kwenye mtandao wa Telegaram, ilikanusha kuwa wanamgambo wake hawakufanya ubakaji wakati wa shambulio la Oktoba 7, 2023 lililofanya nchini Israel.

"Tunapinga vikali na kukemea uratibu wa baadhi ya vyombo vya habari vya Magharibi na kampeni za upotoshaji za Wazayuni zinazoendeleza uwongo usio na msingi na tuhuma zinazolenga kuichafua Palestina, kwamba wanachama wa upinzani walifanya unyanyasaji wa kijinsia wakati wa vita vya mafuriko ya Al-Aqsa," imesema Hamas.

UN inasema timu ya misheni iligundua kuwa katika maeneo mbalimbali nchini Israel, miili kadhaa iliyo nusu uchi au uchi kabisa kutoka kiunoni kwenda chini ilipatikana, wengi wao wakiwa wanawake waliofungwa mikono na kupigwa risasi mara nyingi kichwani.



Uharibifu wa makazi unaotokana na vita kati ya Israel na Hamas unatajwa kusababisha wanawake kuendelea kufanyiwa vitendo vya ukatili baada ya kukosa mahali pa kujihifadhi. **PICHA: MTANDAO**

# SMZ, Benki ya CRDB kutatua vikwazo mikopo ya nyumba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI imeahidi kutatua changamoto zinazokwamisha wananchi wengi kupata mkopo wa nyumba ili kujenga makazi bora, ikiomba sekta binafsi nayo kuangalia namna ya kupunguza masharti na mlolongo mrefu uliopo.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali, alitoa rai hiyo jana alipofungua mkutano wa wadau wa mikopo ya nyumba ulioandaliwa na Benki ya CRDB ili kubadilishana uzoefu kwa kujadili fursa zilizopo na namna ya kunufaika nazo pamoja na kuainisha changamoto na kuziwekea mkakati ya kuzitatua.

"Ninafahamu zipo baadhi ya changamoto ambazo zinastahili kushughulikiwa na serikali, lakini baadhi zinahusu ninyi wadau wa sekta hii. Mwaka jana wastani wa ukubwa wa mkopo, yaani 'mortgage debt size' ulikuwa Sh. milioni 100.3.

"Hiki ni kiwango kikubwa kwa Watanzania wengi kukopesheka. Kwa kutumia uzoefu wenu, ninawaomba mtazame kama kuna uwezekano wa kuwa na dirisha moja la mikopo ya nyumba (one stop center) litakalokuwa na wadau wote muhimu kabla mteja hajaondoka na mkopo anaouhitaji," alisema Waziri Rahma.

Kwa hali iliyopo sasa hivi, waziri alisema kuna wapimaji ardhi, wapangaji miji na benki zinaotoa mikopo ya nyumba kati ya wengi waliopo. Huenda hali hiyo inakuwa kikwazo kwa wananchi wengi kuchukua mkopo wa nyumba kwa kuwa kuna watu wengi sokoni na mlolongo wa kupitia kabla mteja hajamiliki nyumba anayoihitaji.

**Ukipiga gharama hizi kwa kina utaona zinakuwa nyingi na kubwa, hivyo kuwa mzigo kwa mwananchi wa kawaida. Iwapo tutaziunganisha huduma hizi zote pamoja, huenda zikapunguza gharama na kumrahisishia mwananchi kuchukua mkopo wa nyumba ya makazi.**

"Ukipiga gharama hizi kwa kina utaona zinakuwa nyingi na kubwa, hivyo kuwa mzigo kwa mwananchi wa kawaida. Iwapo tutaziunganisha huduma hizi zote pamoja, huenda zikapunguza gharama na kumrahisishia mwananchi kuchukua mkopo wa nyumba ya makazi," alisema Waziri Rahma.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi wa Wateja wa Awali na wa Kati wa Benki ya CRDB, Stephen Adili, alisema benki hiyo inatambua upungufu wa nyumba milioni tatu za makazi uliopo nchini pamoja na mahitaji ya nyumba 200,000 yanayoongezeka kila mwaka ndio maana iliweka mkakati wa kuwa sehemu ya suluhisho la changamoto hiyo.

"Kwa mwaka 2023 pekee kwa mfano, ripoti ya Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania (TMRC) inaonesha jumla ya Sh. bilioni 587.24 zilikopeshwa kwa wateja 5,855 kutoka benki zote 31 za biashara zinazotoa mikopo ya nyumba za makazi.

"Kiasi hiki kingeweza kuongezeka zaidi iwapo wananchi wengi wangekuwa na hati za maeneo na nyumba wanazozimiliki. Tunaiomba serikali iharakishe mchakato wa kutoa hati ambacho ndicho kigezo kikuu, ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya kujenga nyumba za kisasa kwa ajili ya makazi yao," alipendekeza Adili.

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 inaonesha Tanzania Bara majengo ya makazi ni 12,717,893 sawa na asilimia 91.4, majengo ya makazi na biashara ni 470,476 sawa na asilimia 3.4 na majengo ya matumizi mengineyo ni 719,582 sawa na asilimia 5.2. Takwimu hizi zinatengeneza jumla ya majengo 13,907,951 yaliyomo nchini.

Mgawanyo unaonesha kwamba kati ya majengo hayo nchini, 4,132,438 sawa na asilimia 29.7 yako mjini na 9,775,513 sawa na asilimia 70.3 yako vijijini. Kati ya majengo hayo yote, majengo 694,395 sawa na asilimia tano yako katika hatua mbalimbali za ujenzi.

"Kutokana na sababu mbalimbali, Watanzania wengi wanaishi kwenye nyumba za kupanga huku wale wanaojenga wakitumia muda mrefu kukamilisha ujenzi wa nyumba zao kutokana na changamoto za kifedha wanazokutana nazo kwenye safari hiyo. Benki ya CRDB inao wajibu wa kushiriki kuleta suluhisho," alisema Adili.

Katika kiasi chote kilichokopeshwa mwaka 2023, Benki ya CRDB ilitoa jumla ya Sh. bilioni 202.35 ambazo ni sawa na asilimia 34.46 na kunufaisha wateja 1,606 ambao ni sawa na asilimia 28 ya wanufaika wote waliokopeshwa na benki za biashara nchini.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Meneja wa Mikopo ya Nyumba wa Benki ya CRDB, Janerose Mwombela alisema kuna kampuni na taasisi chache zinazojenga nyumba nchini licha ya mahitaji makubwa yaliyopo.

"Licha ya uchache wa nyumba zinazojengwa bado bei ni kubwa kwa wananchi wengi kuzimudu. Ninatoa rai kwa kampuni za ujenzi mwangalie uwezekano wa kujenga nyumba za bei nafuu ambazo wananchi wenye kipato kidogo nao watazimudu," alisema Janerose.

# AYOUB AANZA KUWAKIMBIZA KINA DIARRA KWA 'CLEAN SHEETS'

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa Simba, Ayoub Lakred raia wa Morocco, ameanza kuingia kwenye orodha ya makipa waliokaa mechi nyingi langoni bila kuruhusu bao, akiwakimbiza makipa wengine akiwamo Djigui Diarra wa Yanga, huku Mkongomani Ley Matampi wa Coastal Union, akiwa kinara wa 'clean sheets' kwenye Ligi Kuu Bara mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la Nipashe na zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, Lakred amefikisha 'clean sheets' nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa sawa na makipa Wilbol Maseke wa KMC na Ramadhani Chalamanda wa Kagera Sugar.

Hata hivyo, kwa mujibu wa takwimu zetu, Ayoub amezipata 'clean sheets' hizo baada ya kukaa langoni Simba ikicheza dhidi Coastal Union ikishinda mabao 3-0, Kagera Sugar ikipata ushindi wa mabao 3-0, dhidi ya Tabora United ikashinda mabao 4-0, na JKT Tanzania ikishinda 1-0.

**Kwa sasa ndiye kipa anayeongoza kwa 'clean sheets' kwenye Ligi Kuu kwa upande wa Simba, iliyosheheni makipa mahiri kama Aishi Manula, Ally Salim na Hussein Abel.**

Golikipa wa Yanga, Djigui Diarra raia wa Mali, ana 'clean sheets' sita mpaka sasa kwenye ligi akiwa sawa na kipa wa Geita Gold, Costantine Malimi na chini yao kuna Yona Amosi wa Prisons na Mrundi, Jonathan Nahimana wa Namungo ambao wamekaa langoni mara tano kila mmoja bila kuruhusu bao.

Matampi wa Coastal Union anaongoza akiwa na 'clean sheets' tisa, nafasi ya pili ikishikiliwa na kipa Mnigeria, John Noble, anayekipiga na Klabu ya Tabora United aliyekaa langoni mara saba bila wavu wake kuguswa.



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini jana kabla ya kufunga safari kwenda Morogoro kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Prisons itakayopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini hapo leo. **PICHA: SIMBA**

## Jamhuri yatamba itarejea kivingine

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA timu ya Jamhuri kuendelea 'kujichimbia kaburi' kwenye Ligi Kuu Zanzibar baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-1dhidi ya walinzi wa mipakani, Uhamiaji FC, katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Mau A juzi, imesema itarejea vizuri baada ya mapumziko ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Huo unakuwa mchezo wa tatu mfululizo kwa Jamhuri kushindwa kupata alama tatu na ukiwa ni wa 10 kufungwa kati ya michezo 20 ambayo imecheza hadi sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mfaume Shabaani, alisema wanakwenda mapumziko ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani huku wakienda kusuka mipango itakayowafanya wasalie katika Ligi Kuu.

Alisema timu yake inawachezaji wazuri ambao wanapambana, lakini inakumbwa na tatizo la umaliziaji na nafasi wanazotengeneza.

Alisema mara nyingi wanaposhuka uwanjani wanakuwa na bahati kubwa ya kuutawala mchezo katika vipindi vyote viwili, lakini wanashindwa kupata ushindi kutokana na umaliziaji mbaya kutoka kwa washambuliaji wao.

Aidha, alisema katika kipindi cha kuelekea mapumziko ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa wale wachezaji ambao watakuwapo Kisiwani Pemba yalipo makazi ya timu yao wataendelea na mazoezi mapesi ili kuhakikisha wakirudi uwanjani wanapata matokeo mazuri.

Hata hivyo, aliwatoa hofu mashabiki wa timu hiyo waliopo Wete na Unguja kuwa timu hiyo haitashuka daraja na badala yake waendelee kuipa hamasa ili wachezaji wawe na moyo wa kufanya vizuri na kutimiza lengo lao mwisho wa msimu.

Jamhuri ipo katika mstari mwekundu wa kushuka daraja ikiwa nafasi ya 14 na alama zake 18, baada ya kushinda michezo minne, sare sita na kupoteza 10 kati ya michezo 20 ambayo wamecheza.

# Mollel, Nkya watikisa gofu kumuenzi Lina

**Na Mwandishi Wetu**

NURU Mollel wa Klabu ya Arusha Gymkhana na Fadhil Nkya kutoka Klabu ya Gymkhana Dar es Salaam, wameibuka mabingwa katika michuano ya kumuenzi mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Gofu Lina Nkya, yaliyofanyika viwanja vya gofu vya TPC, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Michuano hiyo ilifanyika juzi iliandaliwa na familia ya Nkya na Chama cha Wanawake Tanzania (TLGU), ikishirikisha wachezaji wengi wa kulipwa na ridhaa kwa ajili ya kumuenzi Lina aliyefariki dunia Januari 19, 2021, ambaye alikuwa kiongozi wa TLGU.

Mollel na Nkya walifungana pointi na kulazimika kurudia shimo moja katika michuano hiyo na kumfanya Mollel kuibuka mshindi kwa pigo moja.

Ushindi huo umemfanya Mollel kuondoka na zawadi ya kitita cha fedha cha Sh. milioni 6.8 huku Nkya akiondoka na Sh. milioni 4.3 na washindi wengine Frank Mwinuka wa Lugalo aliyeondoka na Sh. milioni 2.7 sawa na Isaac Wanyeche wa Kili ya Arusha.

Washindi wengine ni Hassan Kadio aliyepata Sh. milioni 1.2, na wengine wakizawadiwa Sh. 480,000 ambao ni Rajabu Idd, John Said, Salum Dilunga na Elisante Lembric.

Pia, wa ridhaa mshindi wa jumla ni Ally Isanzu aliyezawadiwa Sh. milioni 2.2 na nafasi ya pili ni George Sembi alishinda Sh. milioni 1.3, Isiaka Daud Sh. 900,000, Ibrahim Gabriel Sh. 700,000. Victor Joseph na Elisha Fadhil kila mmoja Sh. 570,000.

Akizungumza wakati wa kufunga michuano hiyo kiongozi wa familia hiyo, Said Nkya (mume wa Lina), aliwashukuru wachezaji wote waliojitokeza katika mashindano hayo na kuwapongeza ambao hawakufanikiwa kushinda akiwahimiza wajitokeze mashindano mengine yanayotarajiwa kufanyika Aprili mwaka huu mkoani Morogoro.

Mchezaji wa kulipwa kutoka Klabu ya Gymkhana, Hassan Kadio, alisema mashindano hayo yamekuwa na ushindani mkubwa mpaka yanamalizika walipatikana wachezaji wa gofu wakulipwa waliofungana pointi.

Naye Jafari Ally ambaye ni mchezaji wa gofu kutoka Klabu ya TPC, alisema mashindano hayo yamekwenda vizuri na wameona vipaji mbalimbali ambavyo vikiendelezwa vitaweza kufanya vizuri katika mashindano mengine ya kimataifa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN AGOMBEWA

KLABU za Manchester United na Paris St-Germain zimeibuka kuwa mstari wa mbele kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 25. ***(Independent)***

### JOELINTON MKATABA MPYA

NEWCASTLE United inakaribia kukubaliana mkataba mpya na Joelinton, huku kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, akiwa amebakiza zaidi ya mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa. ***(Telegrap)***

### HJULMAND AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imetuma maskauti kwenda kumwangalia mchezaji wa Sporting Lisbon, Morten Hjulmand, raia wa Denmark mwenye umri wa miaka 24. ***(Record, via Sun)***

### ZEBRI, AMORIN NA CHELSEA

CHELSEA imewataja makocha wa Brighton, Roberto de Zerbi na Ruben Amorim wa Sporting kama wanaoweza kuchukua nafasi za Mauricio Pochettino. ***(Guardian)***

### TEN HAG KUFUTWA KAZI

WACHEZAJI kadhaa wa Manchester United wanaamini kuwa Kocha wa Uholanzi, Erik ten Hag, atabadilishwa mwishoni mwa msimu huu na wamiliki wenza wapya. ***(Mail)***

### ANGE KUIKATAA LIVER

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, atakataa ofa zozote za kuondoka msimu huu ikiwa ni pamoja na ya kutoka Liverpool. ***(Football Insider)***

### UNITED KUMUUZA SANCHO

MANCHESTER United inakusudia kumuuza winga, Jadon Sancho, 23, msimu huu wa majira ya joto baada ya kipindi chake cha mkopo kumalizika kule Borussia Dortmund, bila kujali kama Erik ten Hag ataendelea kuwa kocha wa United ama la. ***(Football Insider)***

### MINTEH KWA MKOPO

KLABU ya Newcastle inapanga kumpeleka winga wa Gambia, Yankuba Minteh kwa mkopo kwa msimu wa pili mfululizo. Minteh, ambaye Magpies walimsajili kutoka Klabu ya Denmark, Odense Boldklub, kwa pauni milioni sita msimu uliopita, amekuwa katika Klabu ya Feyenoord ya Uholanzi msimu huu. ***(i)***

### ALONSO NA LIVERPOOL

LIVERPOOL huenda ikalazimika kuilipa Bayer Leverkusen ada iliyovunja rekodi ya dunia ya pauni milioni 21 ili kumrejesha Xabi Alonso Anfield msimu huu wa majira ya joto ikiwa ni mara mbili ya ile waliyolipa kumsajili Mhispania huyo kama mchezaji. ***(Mirror)***

### DAVIES KUONGEZEWA OFA

REAL Madrid iko tayari kuongeza ofa yao kwa mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, Alphonso Davies, 23, hadi pauni milioni 43. ***(Cadena Ser, Mundo Deportivo)***

## DONDO SOKA
## MAGAZE LAYA



# NEYMAR KUMFUATA MESSI INTER MIAMI

**MIAMI,** Marekani

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar amesema angependa kucheza tena na Lionel Messi wa Inter Miami katika siku zijazo.

**Wawili hao ni marafiki wazuri na walicheza pamoja kule Barcelona na Paris Saint-Germain, lakini hawatamenyana katika michuano ya Copa America majira ya joto baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil kupata jeraha la goti Oktoba mwaka jana.**

Tangu ilipomsajili Messi katika majira ya joto ya 2023, Miami imewaongeza wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Sergio Busquets, Jordi Alba na Luis Suarez kwenye kikosi hicho.

## ●●● Ningependa kucheza Marekani angalau kwa msimu...

Alipoulizwa kuhusu Messi kuwaleta marafiki zake Inter Miami na kama angependa kucheza naye tena, Neymar aliiambia ESPN Argentina: "Natumai tunaweza kucheza pamoja tena.

"Leo ni mtu mzuri, kila mtu anamfahamu katika soka na nadhani ni mzuri sana, furaha na ikiwa ana furaha, mimi pia."

Fowadi huyo wa Al Hilal, ambaye hatarajiwi kurejea uwanjani hadi Agosti, alihudhuria mashindano ya Formula One Bahrain Grand Prix Jumamosi. Neymar na Messi walishinda mataji ya ligi wakiwa PSG, lakini walishindwa kuleta mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alisema yeye na Messi "waliishi kuzimu" katika muda wao wa pamoja pale PSG.

Wachezaji wote wawili waliondoka katika klabu hiyo mwaka 2023, huku Messi akijiunga na Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), na Neymar akitia saini mkataba wa miaka miwili na Klabu ya Al Hilal inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudia.

Mfungaji bora wa muda wote wa Brazil, Neymar alionesha nia ya kucheza MLS akiwa PSG.

Alipoulizwa mwaka jana kama angependa kustaafu kuichezea Brazil, Neymar alisema kwenye podikasti ya Fenomenos: "Sijui. Nina shaka kuhusu hilo. Sijui kama nitacheza tena Brazil.

"Ningependa kucheza Marekani, kwa kweli. Ningependa kucheza huko angalau kwa msimu mmoja."

# MADRID KUKATA RUFAA KADI YA BELLINGHAM




**MADRID,** Hispania

REAL Madrid itakata rufaa ya kadi nyekundu ya Jude Bellingham dhidi ya Valencia, vyanzo viliiambia ESPN.

Kiungo huyo wa kati wa England alitolewa nje baada ya kipenga cha mwisho cha sare ya mabao 2-2 Jumamosi dhidi ya Valencia kwa madai ya kumtukana mwamuzi.

Ripoti ya mwamuzi ilidai Bellingham alionesha "tabia ya uchokozi" na akapiga kelele mara kwa mara "ni bao letu."

Bellingham ilipiga mpira kwa kichwa akiunganisha krosi ya Brahim Diaz na ulitinga wavuni, lakini mwamuzi Jesus Gil Manzano alipuliza kipenga cha kumaliza mchezo wakati mpira ukiwa angani katika dakika ya tisa ya muda wa nyongeza katika kile ambacho kingekuwa ni ushindi kwa Madrid.

Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alisisitiza baada ya mchezo huo kuwa Bellingham hakumtukana mwamuzi.

"Tulichukizwa na kadi nyekundu ya Bellingham," alisema Ancelotti.

"Hakusema matusi yoyote. Alisema kwa Kiingereza 'ni goli,' lakini alikuwa akisema kile ambacho sote tulikuwa tukifikiria. Mwamuzi aliruhusu mchezo uendelee. Nadhani makosa. Bellingham alikuwa wazi katika kile alichosema.

"Alikuwa na hasira katika majibu yake, lakini hiyo ni kawaida, baada ya kile kilichotokea. Haikuwa tusi, hata kidogo."

# Arsenal mbio moja kwa City, Liverpool



**LONDON,** England

ARSENAL iliifikia rekodi yake ya ushindi mkubwa zaidi wa Ligi Kuu England ugenini kwa kuichapa Sheffield United mabao 6-0 Jumatatu baada ya kufunga mara tano katika kipindi cha kwanza na kupunguza pengo la pointi hadi mbili dhidi ya vinara Liverpool.

Timu hiyo ya Kocha, Mikel Arteta ni ya tatu ikiwa na pointi 61 baada ya michezo 27, pointi moja nyuma ya Manchester City, lakini ikiwa na tofauti nzuri ya mabao kufunga na kufungwa kuliko wapinzani wao wa taji hilo.

'Washikabunduki' hao ndio timu ya kwanza ya Ligi Kuu England kwa kushinda mara saba mfululizo msimu huu na inaonekana kushika kasi kwa wakati ufaao kuweka presha kwenye nafasi mbili za juu.

"Uchezaji mzuri na matokeo makubwa kwetu tena kwa idadi ya mabao tuliyofunga na pasi safi," alisema Kocha wa Arsenal, Arteta kwa furaha.

"Timu inaonesha dalili za kutaka zaidi, chanya sana. Nguvu ni nzuri kwa sasa. Unaposhinda kila kitu ni rahisi, tunapaswa kudumisha kasi sasa."

Arsenal hawakuwa na huruma walipoichambua safu ya ulinzi ya United kwa urahisi tangu mwanzo. Nahodha wa Arsenal Martin Odegaard alifungua lango la uongozi dakika ya tano, kwa shuti kali kutoka katikati ya eneo la hatari baada ya pasi nzuri ya Declan Rice.

"Tumeshinda 6-0 leo (juzi) na hivi karibuni tumeshinda mengi, lakini kazi tunayofanya bila mpira kutoka mbele hadi wavuni ni nzuri sana na ni furaha," alisema Odegaard.

Kulikuwa na taabu zaidi kuja kwa kipa wa United, Ivo Grbic katika usiku ambao alishuhudia majina sita tofauti yakimfunga.

Jayden Bogle alifunga bao lake la kwanza kwa Arsenal dakika ya 13 kabla ya Gabriel Martinelli kufunga dakika mbili baadaye, na kusababisha mashabiki waliochoka wa United kwenda nje ya Uwanja wa Bramall Lane, huku Kai Havertz (dakika ya 25), Rice (39), na Ben White (58) pia wakitikisa wavu.

# Leao hataki kuondoka AC Milan

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Rafael Leao, amesisitiza kuwa hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo siku zijazo, licha ya ripoti za Chelsea na Paris Saint-Germain kumtaka.

Ripoti ya hivi karibuni ilidokeza kwamba Milan inaweza kusikiliza ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, msimu huu wa majira ya joto, huku Chelsea ikitajwa kurudisha nia ya kumtaka Leao.

Paris Saint-Germain pia wametajwa kuwa wanajiandaa na maisha bila Kylian Mbappe na hivyo wanamwania Leao.

Hata hivyo, licha ya uvumi huo, Leao ameweka wazi kuhusu mustakabali wake.

"Mustakabali wangu uko Milan," alisema akiiambia Corriere della Sera. "Nipo hapa na bado nina mkataba wa miaka minne.

"Milan ilinisaidia nikiwa katika hali ngumu sana, walikaa karibu nami, sisahau, mimi ni mwaminifu, nilifika kama kijana, hapa nilikua kama mtu na mchezaji wa mpira. kushinda tena, kichwa changu kiko hapa."

Ingawa Leao alikiri nia yake ya kuwania ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, alisisitiza kwamba kipaumbele kikuu ni kuirejesha Milan kileleni cha mafanikio ya Ulaya.

"Ili kukua, lazima nishinde vitu muhimu, kama vile Ligi ya Mabingwa Ulaya au Ligi ya Europa," alieleza.

"Mambo mazuri husahaulika haraka sana, kwa hiyo lazima ushinde kila mwaka, iwezekanavyo.



## Kriketi waahidiwa mamilioni wakiwika All-African Games

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU za Taifa za Tanzania za mchezo wa Kriketi zimeahidiwa kupewa dola 10,000 (Sh. milioni 25.5), kama zitafanya vizuri kwenye mashindano ya All-African Games, yanayotarajiwa kuanza Ijumaa wiki hii hadi Machi 23, mwaka huu, nchini Ghana .

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mchezo wa Kriketi Tanzania (TCA), Hamis Abdallah, alisema fedha hizo zitagawanya kwenye kwa benchi la ufundi, wachezaji pamoja na viongozi.

"Tumezipa motisha timu zetu, hii imekuja mara baada ya kupatikana kwa uongozi mpya, jambo ambalo linasaidia kutia moyo wachezaji kujituma zaidi," alisema Abdallah.

Aidha, alisema timu zao zipo nje ya nchi zikiendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano hayo ya Afrika, ambapo timu ya wanaume ipo nchini Malasia, wakati ya Wanawake ikiwa Nigeria.

Katibu huyo alisema timu ya wanawake imeondoka jana nchini Nigeria kuelekea Ghana kwa lengo la kujiandaa na mashindano hayo huku ya wanaume ikitarajiwa kuondoka Machi 14, mwaka huu.

Alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakwenda kuipeperusha vema bendera ya taifa kwa kupata matokeo mazuri.

## Benchikha aonya

INATOKA UKURASA 24

hivyo, kwenye kila mchezo lolote linaweza kutokea na ndio maana tutakabiliana nao kwa tahadhari huku tukilenga pointi tatu muhimu," alisema.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea kwenye mchezo huo wa leo na kuwataka wachezaji kusahau matokeo yao na Jwaneng Galaxy na waelekeze akili zao kwenye mchezo wa leo utakaoanza saa 10:00 jioni.

"Ninachoangalia kwa sasa kama kocha ni kuhakikisha kile ambacho tumekuwa nacho, kwa maana ya ubora unaendelea kuwapo kwenye michezo inayofuata tukianza na huu dhidi ya Tanzania Prisons," alisema Benchikha.

Katika michezo minne baada ya mchezo wa leo dhidi ya Tanzania Prisons, Simba itaumana na Coastal Union Machi 9, Singida Fountain Gate Machi 12 na siku tatu baadaye wataumana na Mashujaa FC yote ikichezwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro isipokuwa dhidi ya Coastal Union ambao utapigwa CCM Mkwakwani.

# BARAZA AANIKA TATIZO DODOMA JIJI WAKIIVAA TABORA UNITED LEO



**Na Saada Akida**

KIPIGO cha mabao 4-1 ilichokipata dhidi ya Azam FC mwishoni mwa wiki, kimetokana na makosa binafsi ya wachezaji wake hususan safu ya ulinzi, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Francis Baraza, ambaye amesema wanatarajia kusahihisha makosa yao dhidi ya Tabora United leo.

Dodoma Jiji FC ambayo ilikubali kichapo hicho katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, kabla ya mchezo huo pia ilitoka kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union.

**Akizungumza na Nipashe juzi, Baraza alisema licha ya mechi hiyo dhidi ya Azam FC kuzidiwa kwenye safu ya kiungo, lakini wachezaji wake wanafanya makosa binafsi katika safu yake ya ulinzi jambo ambalo limewafanya kupoteza mechi mbili kati ya tatu ambazo wamecheza hivi karibuni.**

Alisema wamerudia Dodoma kujianda na mechi dhidi ya Tabora United na Geita Gold FC, kuhakikisha wanapunguza makosa waliyoyafanya katika mechi zilizopita.

"Tunafanyia kazi makosa yetu ikiwamo kusahihisha makosa ya mchezaji mmoja mmoja na kuwajengaa kisaikolojia huku tukiendelea kuwapa mbinu na ufundi ili kufanya vizuri katika mechi hizo mbili tutakazocheza nyumbani," alisema Baraza.

Aliongeza kuwa licha ya kupata siku moja ya maandalizi, ametumia muda kuo kusahihisha makosa yao kabla ya leo kucheza mechi yao dhidi ya Tabora United na Jumamosi wiki hii kucheza na Geita Gold FC, zote wakiwa nyumbani katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

## MWENDO WA 6-0...




Nahodha wa Arsenal, Martin Odegaard, wakipongezana na kipa wa timu hiyo, David Raya, baada ya Arsenal kuichapa Sheffield United mabao 6-0, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Bramall Lane, usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

## *TFF yatoa siri Simba, Yanga kuwika CAF*

INATOKA UKURASA 24

nchini Ivory Coast, ambapo Tanzania ilikuwa kwenye kundi moja na Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Morocco kuwa Taifa Stars haikufanya vibaya sana na nusura iende hatua ya 16 bora, kwa sababu Stars, ilikuwa kundi moja lenye timu zenye wachezaji wanaowafahamu.

"Wachezaji wetu waliihofia Morocco tu, lakini siyo Zambia kwa sababu ilikuwa na wachezaji wanaocheza nao kila wiki (Clatous Chama na Kennedy Musonda), na DR Congo (Henock Inonga), na hiyo ndiyo faida ya kuwa na wachezaji wa kigeni, inawaimarisha hata wachezaji wa Kitanzania kwenye timu yetu wa Taifa Stars," alisema.

Aidha, aliwapongeza pia wadhamini mbalimbali wa ligi ambao wataonyesha mechi zote 240 za Ligi Kuu, akisema hayo ni maendeleo makubwa ya soka kipindi cha uongozi wake, ambapo sasa wachezaji wa timu zote 16 za Ligi Kuu na wa chini ya miaka 20 wanalipwa mishahara.

## Yanga yaitaka Asec

INATOKA UKURASA 24

"Kwa tuliyopitia katika hatua ya makundi hatuna presha juu ya yeyote kati ya hao kwa sababu tumecheza na Al Ahly na CR Belouizdad ambao ni timu bora na Yanga imefanikiwa kuingia robo fainali mbele ya Waalgeria," alisema Kamwe.

Kuhusu kucheza nusu au fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kama ilivyotokea msimu uliopita kwenye Shirikisho, Kamwe alisema lazima ukweli usemwe kucheza fainali shirikisho ni tofauti na michuano waliyopo sasa.

"Mashabiki wa soka sio wajinga na kwamba hawajui mpira, hii michuano tuliopo sasa ni mingine, kumbuka imepita miaka 25 Yanga haijacheza makundi Ligi ya Mabingwa ndiyo sasa, hivi leo uwaambie watu tutabeba ubingwa, hilo haliwezekani.

"Hatuna historia nzuri katika michuano hii ya Ligi ya Mabingwa, sasa hivi tupo robo fainali hatuwezi kusema yaliyo mbele yetu kwa sababu hatujui tutakutana na nani licha ya kuwatamani Asec Mimosas," alisema Kamwe.

# Michezo

Jumatano Machi 6, 2024

Nipashe




Real kukata rufaa kadi ya Bellingham UKURASA 22

# TFF yatoa siri Simba, Yanga kuwika CAF

## ●●● Yajivunia mafanikio hayo huku ikisifu wachezaji wa kigeni kwa...

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, amezipongeza Klabu za Simba na Yanga kwa kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, akisema wameipa sifa nchi, na kwake binafsi wamemheshimisha mbele ya viongozi wa mashirikisho mengine Afrika na dunia, lakini akitoa siri ya mafanikio hayo.

**Kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo, timu za Simba na Yanga zimetinga kwa pamoja hatua ya robo fainali huku Tanzania ikiwa nchi pekee iliyoingiza timu mbili katika hatua hiyo.**

Mara nyingi imezoeleka kuona nchi za Kaskazini maarufu nchi za Kiarabu husussan Misri, Morocco na Tunisia zikiingiza timu mbili katika hatua hiyo, lakini safari hii ni Tanzania pekee iliyofanikiwa kufanya hivyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Karia, alisema hayo yote yametokana na kuigeuza ligi ya Tanzania kutoka kuwa ya ridhaa na kuwa ya kulipwa na ya kibiashara zaidi, hali iliyosababisha kuja kwa wachezaji wengi wa kigeni na wenye ubora mkubwa.

"Nazipongeza Klabu za Simba na Yanga, kuanzia viongozi na wachezaji wao, kuingia kwao hatua ya robo fainali kumeiheshimisha nchini yetu, ni Tanzania pekee iliyoingiza timu mbili msimu huu, wameniheshimisha mimi kama Rais wa TFF mbele ya viongozi wenzangu na Mashirikisho ya Soka Afrika na duniani kwa jumla.

"Pia napelekeza pongezi zangu kwa wachezaji wa kigeni wa Simba na Yanga kwani wamezifikisha timu hizo hapo na wamewabadilisha hata wachezaji wetu wa Kitanzania," alisema Karia.

Alisema awali walipoweka idadi ya wachezaji 12 wa kigeni walipata upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya wadau wa michezo, lakini kwa sasa matunda yake yanaonekana.

"Tuliruhusu wachezaji 12 wa kigeni ili mradi tu tukaweka vigezo wawe wa viwango gani, tulipata upinzani mkali, lakini leo tunaona, ni hao hao kwa kiasi kikubwa wamezisaidia timu hizi za Tanzania ambapo sidhani kama tungekuwa na Watanzania watupu tungeweza.

"Lakini hawa wachezaji wa kigeni wamesaidia hata kuwaimarisha wachezaji wetu kwa sababu kila wiki wanacheza nao hapa kwenye ligi, kwa hiyo hata wakichaguliwa kwenye timu ya taifa wanakuwa hawana woga nao kwa kuwa wamewazoea," alisema Karia.

Alikumbushia michuano ya AFCON iliyoisha hivi karibuni

INAENDELEA UKURASA 23




# Yanga SC yaitaka Asec robo fainali

**Na Saada Akida**

WAKATI droo ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikitarajiwa kupangwa Jumanne ya wiki ijayo, Klabu ya Yanga, sala zao wameziele-keza kwa Mungu wakiomba wapangwe na Asec Mimosas ya Ivory Coast ambayo ni kinara wa Kundi B, lililokuwa likizijumuisha Wydad Casablanca ya Morocco, Jwaneng Galaxy ya Botswana na watani wao wa jadi, Simba.

Katika kundi hilo, Simba imefuzu kwa kushika nafasi ya pili sawa na Yanga ambayo ilikuwa Kundi C, iliyopita na vinara Al Ahly, huku CR Belouizdad ya Algeria na Medeama ya Ghana zikishindwa kupenya robo fainali.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe, ameweka wazi kuwa wanaomba Mungu wakutane Asec Mimosas ya Ivory Coast katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika .

Amesema kati ya timu tatu Petro de Luanda ya Angola, Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini) na Asec Mimosas ambao mojawapo wanaweza kupangwa nayo, wao wanaitaka miamba hiyo ya Ivory Coast.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamwe, alisema hata kama watapangwa na timu tofauti na Asec Mimosas, wanaamini wanaweza kufanya vizuri kutokana na ubora waliokuwa nao.

"Tuko tayari kukutana na yeyote katika hatua inayofuata, lakini ingetupendeza tukakutana na Asec Mimosas ambao walionekana bora katika kundi lao, sisi Yanga tunataka pia kuwaonyesha Simba kuwa hao ni wabovu kwa kumfunga na kuwaonyesha ubora wetu.


Gamondi

INAENDELEA UKURASA 23

# Benchikha aonya mechi Prisons leo

**Na Faustine Feliciane,** Morogoro

KOCHA wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema hawataidharau Tanzania Prisons wanaokutana nao leo kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Simba leo inakutana na Tanzania Prisons huku ikiwa imetoka kupata ushindi mnono kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika wa mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na kufuzu robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema matokeo na sherehe ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imemalizika baada ya dakika 90 za mchezo wao na Jwaneng na sasa akili yao ipo kwenye michezo ya Ligi Kuu kwa kuanzia na mechi ya leo dhidi ya Tanzania Prisons.

"Sitarajii kuwa utakuwa mchezo mwepesi, lazima turudi haraka kwenye hali yetu ya kutaka pointi tatu katika michezo yote iliyobaki ya Ligi Kuu, tumefuzu hatua ya robo fainali CAF, lakini hiyo imeisha mara baada ya mchezo. Kwa sasa tunataka kuendeleza kasi yetu ya kuwania ubingwa wa Tanzania, ili tufikie huko ni lazima sasa kuhakikisha tunashinda michezo yetu yote," aisema Benchikha, na kuongeza,

"Hatuwezi kuwadharau Tanzania Prisons kwa kuwa sisi tumetoka kufanya vizuri kwenye mechi ya kimataifa, mpira haupo

INAENDELEA UK.23


Benchikha

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >